# Nipashe

Jumanne Septemba 13, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581067

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 11


SUPA JACKPOT

TZS. 1,031,243,893

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Uzito uliokithiri tishio, wengi wana maradhi

UKURASA 3



# Kilio maumivu tozo chasikika

• **Samia** ampa maelekezo maalum Mwigulu, ACT yataka uwazi matumizi yake... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### HATI YA MASHTAKA YAMKWAMISHA SABAYA

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi, inayomkabili aliyekuwa Mkuu...



UKURASA WA 5

### MAMBO MATATU KUTIKISA BUNGE

MKUTANO wa nane wa Bunge la 12, unaanza leo...



**Hili ni jambo jema sana na ni mapendekezo yangu kwamba ianze na matibabu ya afya tu kwanza, isianze na mambo mengi, hayo mengine yatafanyika huko kwingine.**

Kibamba



**Bima ni nzuri sana ila kuwe na mfumo maalum wa kidijitali utakaosaidia kudhibiti ubadhirifu wa aina yoyote kila kitu kiendeshwe kidijitali, ili kila kitu kinachofanyika kiwe kinaonekana kwa urahisi.**

Kitwanga



**Ni muhimu bima ichukuliwe kwa umuhimu wake. Isiingiliwe na serikali mamlaka yake iwe yake tu na fedha yake isichukuliwe kufanyia vitu vingine hata zikijaa ziachwe tu.**

Bisimba

# Serikali yapewa angalizo Bima ya Afya kwa Wote

UKURASA 7

## Macho yote kwa Kenyatta akikabidhi kiti kwa Ruto leo



UKURASA 19

**MICHEZO** YANGA YAMWAGIWA BILIONI 10/- UK.24

**KABWELA** UK.18

HABARI KITAIFA

# Kilio maumivu tozo chasikika

**Na Waandishi Wetu,** TARIME

KILIO dhidi ya maumivu ya tozo za kielektroniki kimesikika baada ya jana Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuweka wazi kuwa amepokea maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuhusu kushughulikia malalamiko ya wananchi yaliyojitokeza kuhusu gharama za tozo hizo ili kuleta unafuu wa wananchi.

Dk. Nchemba alibainisha hayo kwa nyakati tofauti jana wilayani Tarime mkoani Mara alipozuru kikazi kutembelea mpaka wa Tanzania na Kenya katika Mji wa Sirari na kuzungumza na wananchi, wafanyabiashara na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato (TRA).

Alisema wataalamu wa wizara yake wanayafanyia kazi maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na Rais, chama pamoja na maoni ya wananchi kuhusu jambo hilo na kuahidi kuwa muda si mrefu serikali itakuja na majawabu baada ya kufanya marekebisho kadhaa ili kuleta unafuu.

Dk. Nchemba alisema kuwa nia ya serikali ni kuhakikisha ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo unakwenda sambamba na kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuweka miundombinu wezeshi inayolenga kuibua wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa na hatimaye kuinua kipato cha mwananchi mmoja mmoja.

"Serikali imepokea maoni ya Watanzania wakati wa kutekeleza nia hii njema ya serikali kwa wananchi wake na kwa hiyo baada ya kupokea maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu kuyazingatia maoni ya wananchi yanayoendelea kutolewa, tunalifanyia kazi suala hilo na punde tutaleta majawabu," aliahidi huku akishangiliwa na wananchi wa Sirari waliokusanyika kumsikiliza.

Waziri huyo alisema kuwa serikali inahitaji fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati pamoja na miradi mingine ya huduma za jamii ambayo pia inahitaji fedha na ndiyo maana kuna kile alichokiita 'kugusana gusana' (tozo) kwa wale wenye unafuu ili kushiriki kuchangia maendeleo hayo.

Aliitaja baadhi ya miradi ambayo haiwezi kusimama kwa kukosa fedha ni pamoja na ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere unaogharimu zaidi ya Sh. trilioni 6, ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) unaogharimu zaidi ya Sh. trilioni 23, upanuzi wa bandari, miradi ya TARURA, ujenzi wa hospitali na vituo vya afya, Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Malipo, ujenzi wa vyumba vya madarasa, mabweni na nyumba za walimu na ujenzi wa vyuo vya ufundi.

Dk. Nchemba alisema shughuli zingine muhimu ambazo haziwezi kusimama ni ulipaji wa mishahara kwa watumishi, kugharamia miradi ya kilimo ikiwamo utoaji ruzuku kwenye mbolea, utoaji wa ruzuku ya mafuta ili kukabiliana na mfumuko wa bei na miradi mingine inayoendelea kutekelezwa katika maeneo mbalimbali nchini ambayo inahitaji fedha nyingi.

Aliwaomba Watanzania kuendelea kuiunga mkono serikali yao na kumwombea afya njema Rais Samia kwa kuwa ana nia njema ya kuharakisha maendeleo ya wananchi na amefanya hivyo kwa vitendo katika kipindi kifupi alichoshika madaraka ya nchi ambapo miradi mbalimbali ya kimkakati na ya kijamii imetekelezwa kwa kiwango ambacho hakijawahi kutokea kabla yake.

Alitolea mfano wa baadhi ya miradi inayokusudiwa kutumia fedha zitakazopatikana kwenye tozo kuwa ni ujenzi wa vyumba vya madarasa vipatavyo 17,000 kabla ya Januari 2023 pamoja na ujenzi wa vyuo vya ufundi katika wilaya 72 ambazo hazina vyuo hivyo ambapo jumla ya Sh. bilioni 200 zitatumika kujenga vyuo hivyo.

Kuhusu mazingira ya ufanyaji biashara katika mpaka wa Sirari na Mkoa wa Mara kwa ujumla, Dk. Nchemba aliiagiza TRA kuhakikisha inafanya kazi yake ya kukusanya kodi bila kuathiri biashara za wananchi na kuacha kutumia mabavu kukusanya kodi hizo. Aliwaomba wananchi kushiriki katika maendeleo ya taifa lao kwa kulipa kodi kwa hiari na kuwafichua wafanyabiashara wasio waaminifu wanaofanya magendo na hivyo kuikosesha serikali mapato na kuathiri mwenendo wa uchumi kwa kuleta ushindani usio sawa.

Aliahidi kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria mbalimbali za kodi zinazokwaza ukuaji wa biashara nchini ili kuikuza sekta hiyo, kuzalisha ajira na kukuza uchumi wa nchi.

Dk. Nchemba pia aliwataka wafanyabiashara kuacha kufanya biashara za magendo mipakani kwa kuwa serikali haiwezi kuhalalisha biashara hiyo.

Awali wabunge wa Mkoa wa Mara, wakiwamo wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, Viti Maalum Mkoa wa Mara, Ghati Chomete, wa Tarime Mjini, Michael Kembaki na wa Serengeti, Dk. Jeremiah Amsabi, waliwasilisha kero za wananchi wa mkoa huo, ikiwa ni pamoja na uhusiano duni baina ya askari polisi, Jeshi la Uhamiaji na TRA, hali waliyosema inakwaza ustawi wa wananchi na wafanyabiashara wa eneo hilo hususan wanaoishi katika mpaka wa Tanzania na Kenya wa Sirari.

Miongoni mwa kero hizo ni kukamatwa kwa wananchi wakiwa na bidhaa wanazonunua Kenya kwa bei nafuu kulinganishwa na bei ya nyumbani ikiwamo saruji, mabati, sukari, mbolea na baadhi ya bidhaa ndogo ambazo wananchi wanazipata kutoka Kenya lakini wakiziingiza Tanzania, hata kama ni mabati 10 au mifuko miwili ya saruji, wanakamatwa.

Akiwa ameambatana na Kamishna wa Idara ya Sera kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Elijah Mwandumbya, Waziri Nchemba alitembelea Kituo cha Forodha cha Pamoja cha Sirari na kuzungumza na wafanyakazi wa TRA katika mpaka huo.

**ACT NA UWAZI**

Wakati hayo yakiendelea Wizara ya Fedha, Chama cha ACT-Wazalendo kimeitaka serikali kuweka wazi mchanganuo wa makusanyo na matumizi ya fedha zote zinazotokana na miamala ya simu na benki.

Chama hicho pia kimetaka mchanganuo wa matumizi ya mkopo wa fedha za UVIKO-19 uliochukuliwa na serikali kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) uwe wazi ili kuondoa kile kilichouita utata.

Mkoani Dar es Salaam jana, Msemaji wa Sekta ya Fedha na Uchumi wa chama hicho, Emmanuel Mvula, alisema serikali imetoa taarifa ya matumizi ambayo haijaeleza kwa kina ni kiasi gani na mgawanyo wake badala yake kumekuwa kukitolewa taarifa ya matumizi ya jumla.

Septemba Mosi mwaka huu, Waziri Nchemba alisema makusanyo ya tozo za kielektroniki kwa mwaka 2021/22 yalitumika kujenga vituo vya afya, madarasa na barabara.

Mvula alihoji kama fedha hizo zilitumika kujenga vituo vya afya, vyumba vya madarasa na barabara, zilizokopwa zilifanya kazi gani, huku akiitaka serikali kusitisha tozo hizo kwa kuwa ni maumivu kwa wananchi.

"Tunapinga utitiri huu wa tozo na tunaitaka serikali iweke wazi makusanyo na matumizi yote ya fedha zinazopatikana kutokana na miamala ya simu na benki kwani tozo hizo zinaathiri sana uchumi wa wananchi.

"Tozo zinashusha hamasa kwa wananchi kutumia mifumo ya kisasa ya kuweka fedha na watarudisha mfumo wao wa zamani wa kuweka fedha majumbani," alitahadharisha.

Mvula aliitaka serikali kutoa ufafanuzi kuhusu fedha ambazo zimetumika kujenga vituo vya afya, madarasa na barabara kwa kuwa kuna fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na IMF Oktoba mwaka jana ambazo zilitolewa ufafanuzi wa matumizi hayo hayo.

"Waweke wazi matumizi ya hizo tozo zilizokusanywa kupitia miamala ya kibenki, waseme hizi tumejenga kwa tozo za kielektroniki na hizi tumejenga kwa fedha za UVIKO-19," alisema.

Mvula pia alisema chama chao kinashauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) afanye ukaguzi maalum wa makusanyo na matumizi ya fedha zilizopatikana kutokana na tozo ya miamala ya simu na benki katika kuchagiza ujenzi wa vituo vya afya.

"Tunamshauri CAG kufanya ukaguzi maalum, aangalie ubora na thamani ya hivyo vituo vya afya pamoja na mapato ya fedha hizo," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Innocent Bashingwa, katika ufafanuzi wake hivi karibuni, alisema Sh. bilioni 117 za tozo zimetumika kujenga vituo vya afya 234 kwenye tarafa na kata na Sh. bilioni 145.5 zilitumika katika ununuzi wa vifaa tiba huku miradi ya elimu ikigharimu Sh. bilioni saba.

***Imeandikwa na Beatrice Mwaigomole na Said Muhibu (SAUT), Fatuma Athumani na Golden Kisapile (TUDARCo)**

# Samia ashauri kuwekeza kwenye rasilimali watu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema nchi za Afrika zinapaswa kuwekeza katika rasilimali watu hususan elimu kwa vijana ili kuwa na maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Sambamba na hayo, amesema maendeleo ya Bara la Afrika yatapatikana haraka iwapo wanawake na vijana watawezeshwa kwa mitaji na taasisi za fedha pamoja na kuwaondolea vikwazo vya kibiashara hasa katika maeneo ya mipakani.

Samia alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa siku tatu wa Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA) kuhusu uwezeshaji wanawake na vijana katika biashara Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Mkutano huo wenye kaulimbiu "Wanawake na Vijana: Injini ya Biashara ya AfCFTA Barani Afrika", ni wa kwanza kufanyika tangu kuanzishwa kwa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika.

Alisema Afrika inahitaji nguvu kazi imara katika maendeleo ya kiuchumi, hivyo uwekezaji katika elimu kwa vijana ni muhimu kwa kuwa sababu kubwa ya nchi nyingi zilizopiga hatua kimaendeleo ziliwaendeleza vijana kielimu.

Rais Samia alitoa mfano wa China ambayo alisema maendeleo yake yanachangiwa na kuwa na vijana wenye ujuzi hasa katika sayansi na teknolojia, hivyo nchi za Afrika hazina budi kuwekeza kwa vijana katika elimu ikiwamo ubunifu katika nyanja mbalimbali.

"China ni nchi ambayo inapigiwa mfano kwa maendeleo na siri kubwa ni uwekezaji iliyofanya kwa vijana. Kampuni nyingi zinazofanya vizuri zinaongozwa na vijana wenye umri wa miaka 18 hadi 35 pamoja na matumizi ya sayansi na teknolojia.

"Afrika inaweza pia kujenga uchumi imara kwa kuwekeza zaidi kwa vijana katika elimu hasa sayansi. Kwa kufanya hivi tutapiga hatua kubwa kiuchumi," alisema.

Pia alisema njia nyingine katika kufikia malengo ya maendeleo ni kuondoa vikwazo vinavyowakabili wanawake na vijana. Sambamba na hiyo, alisema mabadiliko ya kisera na kisheria yanapaswa kufanywa ili kutimiza azma hiyo.

"Wanawake na vijana wanakumbana na vikwazo mbalimbali katika biashara zao hasa maeneo ya mipakani hasa mambo ya leseni na vibali.

"Tunashukuru kwa Afrika Mashariki tumepunguza tatizo hili kwa kiasi kikubwa, hivyo ni changamoto kwetu kuanzia maeneo ya kikanda na baadaye bara zima la Afrika kuondoa vikwazo hivi," alisema.

UWEZESHAJI WANAWAKE

Rais pia alisema Tanzania imeanza kuondoa vikwazo mbalimbali ambavyo vinawakwamisha wanawake na vijana katika biashara na masuala mengine ya maendeleo vikiwamo ukosefu wa mikopo yenye masharti na riba nafuu kutoka taasisi za fedha, sera na ubaguzi na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake.

"Katika masoko kwa mfano tumebaini kwamba hakuna maeneo ambayo wanawake wanaweza kutunzia watoto wakati wanafanya biashara na tumeanza kulitafutia ufumbuzi hili. Mwanamke anabeba mtoto kutwa nzima akiwa sokoni anafanya biashara, hili si zuri.

"Lakini suala la usawa wa kijinsia katika biashara linafanyiwa kazi. Kuna unyanyasaji wa kijinsia katika biashara kwamba baadhi ya kazi ni za wanaume tu pia wanawake wamepewa majina mabaya ambayo ni unanyasaji," alisema.

Kuhusu ununuzi wa umma, alisema serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuziwezesha kampuni za vijana na wanawake kutoa huduma serikalini. Alisema lengo ni kufikia asilimia 30 ya kampuni zinazomilikiwa na wanawake na vijana kutoa huduma hizo.

"Kuna miradi mingi ya maendeleo kama vile ujenzi wa barabara vijijini. Asilimia 30 au zaidi ya kazi hizi tutatoa kwa wahandisi na makandarasi wanawake ikiwa uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na kuleta maendeleo endelevu," alisema.

**MATUMIZI YA RASILIMALI**

Rais Samia alisema Afrika pia inatakiwa kutumia rasilimali zilizopo kwa ajili ya kujiletea maendeleo. Alizitaja baadhi ya rasilimali hizo kuwa ni maliasili, madini, mifugo, ardhi kwa ajili ya kilimo.

Alisema Afrika ina utajiri wa rasilimali lakini ni bara lenye watu wengi maskini kwa sababu rasilimali zilizopo hazitumiki ipasavyo badala yake zinanufaisha watu wa nje, hivyo wakati umefika wa kutumika kwa maendeleo yake.

Katika muktadha wa uwezeshaji wanawake na vijana, Rais alisema fursa hizo zinapaswa kutumiwa kikamilifu na makundi hayo ili kuleta maendeleo endelevu hususan katika uongezaji wa thamani.

Rais pia alisema nchi za Afrika zinatakiwa kuainisha fursa za kisera zitakazowawezesha wanawake na vijana kunufaika ipasavyo katika soko la ndani, kikanda na kimataifa.

HABARI KITAIFA

## Viongozi Afrika wataja sifa kuzingatia usawa kijinsia

Na Mwandishi Wetu

VIONGOZI wa Afrika wametaja mambo mbalimbali yatakayowawezesha wanawake na vijana kuwa na maendeleo ikiwamo kuwa na sera na sheria zinazozingatia usawa baina ya wanaume na makundi maalumu yakiwamo ya wanawake na vijana.

Viongozi hao ambao ni marais na makamu wa rais wanawake walioko na waliokuwa katika nafasi hizo kwenye nchi mbalimbali za Afrika, walitaja mambo hayo walipozungumza katika mkutano wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), unaoendelea jijini Dar es Salaam.

Walisema uwekezaji katika makundi hayo na kuwa na biashara jumuishi ni mambo muhimu kwa maendeleo endelevu ya Afrika.

Rais wa zamani wa Malawi, Dk. Joyce Banda, alisema utashi wa kisiasa miongoni mwa viongozi wa Afrika ni jambo la msingi katika kuleta maendeleo kwa wanawake na wanaume pamoja na jamii kwa ujumla.

Alisema jambo la muhimu ni kwa nchi za Afrika kujenga uchumi imara utakaowawezesha wanawake kuondokana na umaskini.

"Ni lazima tufungue fursa zitakazowawezesha wanawake na vijana ili wasidhalilishwe na kunyanyaswa. Vijana wetu wanaofia katika Bahari ya Mediterranean na mabinti wanaodhalilishwa Mashariki ya Kati ni matokeo ya umaskini katika Afrika.

Ni wakati sasa wa kuwawezesha wanawake na vijana ili washiriki katika mchakato wa maendeleo kwa kuwa na sera na fursa zitakazowaondoa katika umaskini. Kama wanawake hawatashirikishwa kikamilifu katika mchakato wa maendeleo, Afrika haiwezi kuwa na maendeleo," alisema.

Makamu wa Rais wa Liberia, Jewel Howard Taylor alisema uchumi jumuishi ikiwamo kutoa kipaumbele kwa wanawake na vijana ni muhimu kwa sababu makundi hayo ni kiungo muhimu kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Alisema wanawake na vijana wanapaswa kuwa na uhuru na haki katika masuala ya kifedha ikiwamo mikopo katika taasisi za fedha, fursa za kiuchumi pamoja na kuondoa vikwazo vinavyowakabili kama ukatili wa kijinsia na sheria kandamizi.

Taylor alisema asilimia 70 ya shughuli za kiuchumi Afrika zinafanywa na sekta isiyo rasmi na idadi kubwa ya wanaofanya ni wanawake na vijana. Alisema makundi hayo yanapaswa kuwekewa mazingira, sheria na sera rafiki ili kuleta maendeleo endelevu ya Afrika.

Jessica Alupo, Makamu wa Rais wa Uganda, alisema wanawake na vijana ni nguzo muhimu kwa maendeleo ya Afrika, hivyo wanapaswa kupewa kipaumbele katika uwezeshaji ikiwamo huduma za kifedha.

Alisema wanawake na vijana wanapaswa kushirikishwa kikamilifu katika masuala ya maendeleo kupitia sekta mbalimbali kama vile kilimo, biashara, teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), uzalishaji na huduma.

# Uzito uliokithiri tishio

Na Augusta Njoji, DODOMA

WIZARA ya Afya imesema hatari ya watu kupata tatizo la uzito uliopindukia imeongezeka kwa asilimia 73 kwa kipindi cha miaka 10 nchini hali inayochochea magonjwa yasiyo ya kuambukiza (NCD).

Pia imesema theluthi mbili ya watu wenye magonjwa yasiyo ya kuambukiza hawajijui huku wengine wanafika hospitali wakiwa wameshapata madhara.

Kutokana na hali hiyo, wizara hiyo imekuja na mkakati wa kuifikia jamii na kutoa elimu kufuata mtindo bora wa maisha sambamba na mwongozo wa kukabiliana na tabia bwete.

Akizungumza jana kwenye kikao cha Waratibu wa Mikoa wa NCD na waandishi wa habari kilichofanyika kwa njia ya mtandao, Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia magonjwa yasiyo ya kuambukiza kutoka Wizara ya Afya, Dk. James Kiologwe, alisema mzigo wa magonjwa hayo umekuwa ukiongezeka nchini mwaka hadi mwaka na takwimu za mwaka 2009 hadi 2019 zinaonesha hali hiyo.

"Yaani kichocheo cha uzito uliopindukia kimeongezeka kwa takribani asilimia 73, changamoto zinazotokana na lishe zimeongezeka kwa takribani asilimia 32, vihatarishi vinavyotokana na tumbaku vimeongezeka kwa asilimia 14, vihatarishi vinavyotokana na matumizi ya pombe vimeongezeka kwa asilimia 15.9," alisema.

"Sababu kubwa ni kuongezeka kwa vichocheo hatarishi vya magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambapo tafiti zimeonesha kwamba katika kipindi cha miaka 10 tu visababishi vya magonjwa vimeongezeka sana hasa kwa magonjwa yasiyoambukiza ikilinganishwa na vile vya magonjwa ya kuambukiza," alisema.

Alibainisha kuwa hatari hiyo inatokana na ulaji usiofaa kwa kula chakula kuzidi mahitaji ya mwili na hivyo kunenepa, kutofanya mazoezi, matumizi ya pombe, tumbaku, msongo wa mawazo na kutopata usingizi wa kutosha. Dk. Kiologwe alisema kutokana na vihatarishi na mzigo wa magonjwa hayo kuongezeka, wizara imeona ni muhimu kupata elimu shi wa habari kutoa elimu sahihi.

"Kuna elimu nyingi huko hazipo sahihi zinakinzana na changamoto za kibiashara na kiviwanda nazo ni muhimu kupata elimu sahihi maana huku tunazungumza kuhusu madhara ya unywaji pombe na sigara kupita kiasi au sigara kuna wengine wanahamasisha hivyo ni lazima tuwe na timu kubwa ambayo itatusaidia kufikisha elimu sahihi," alisema.

Alisema kikao hicho kinatumika kuunda timu kwenye mikoa za kupambana na magonjwa hayo na wanatarajia kuwa na tuzo kwa ajili ya waandishi wa habari watakaoandika habari za magonjwa hayo.

Kuhusu tatizo la magonjwa hayo kwa vijana, Mkurugenzi huyo alisema kuna asilimia 18 ya vifo vya mapema kwa watu wenye miaka 30 hadi 60 na kwamba hali hiyo inatokana na mtindo wa maisha wanaoishi.

Kwa upande wake, Katibu wa kikao hiko, Goodluck Tumaini, alisema kama mtu mwenye tatizo la figo linalomlazimu kusafisha damu mara tatu kwa wiki, mwajiri atakuwa anakosa nguvu kazi hiyo kwa siku tatu.

"Mathalani gharama anazopata mtu huyu anatumia hadi Sh. 300,000 kwa mchujo mmoja wa damu maana yake kwa wiki Sh. 900,000 ni mzigo mkubwa kwa jamii na kwa familia na taifa kwa jumla na Mfuko wa Bima ya Afya kwa kuzingatia hili tumeona tuje na mkakati wa kufikia jamii kuwa na waandishi watakaoshirikiana na waratibu kuifikia jamii," alisema.




Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, mkoani Kilimanjaro, kwa kesi namba 2 ya mwaka 2022, kufuatia wenzake wanne kuachiwa huru wiki iliyopita baada ya kukiri makosa na kulipa faini ya Sh. 50,000 kwa kila kosa kwa makosa mawili kila mmoja pamoja fidia ya Sh. milioni moja kila mmoja kwa mwathirika wa tukio. PICHA: MARY MOSHA

## Hati ya mashtaka yakwamisha kesi ya Ole Sabaya

Na Mary Mosha, MOSHI

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi, inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, umeishangaa Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP), kushindwa kutoa kibali kwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi kusikiliza kesi hiyo, licha ya kuruhusu washtakiwa wanne kufanya makubaliano na baadaye kuachiwa huru.

Upande wa utetezi umeendelea kuitupia lawama ofisi ya DPP, kwa madai ya kushindwa kuifanyia marekebisho hati ya mashtaka ambayo imewaondoa washtakiwa wanne.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Salome Mshasha, Wakili wa Utetezi, Hellen Mahuna alidai makahakamani kuwa hati ya mashtaka iliyosomwa inawataja washtakiwa watano licha ya uhalisia anaonekana yupo mmoja (Sabaya).

"Mheshimiwa hii inaonesha DPP, anafanya masuala vile anataka, hati iliyosomwa na wakili msomi, Sabitina Mcharo inataja washtakiwa watano licha ya wanne kuachiwa wiki iliyopita, upande wa utetezi hauna pingamizi juu ya walioachiwa, ila bado tunahoja za malalamiko ambayo yanatupelekea kuona ofisi ya DPP kushindwa kutekeleza majukumu yake licha kuomba mara kwa mara hapa," alidai.

"Mshtakiwa wa kwanza (Sabaya) ni mgonjwa na anapaswa kujua haki zake, tuna imani mahakama yako kwa kutoa haki," alisema.

Wakili Hellen akiambatana na wakili Fauzia Mustapher, waliieleza kushangazwa na DPP kuruhusu kufanyika kwa 'Pre Bargaining' na kushindwa kuruhusu mahakama hiyo kuanza kusikilizwa kwa kesi hiyo.

"Mheshimiwa, niombe mahakama yako tukufu ielekeze Jamhuri kukamilisha upelelezi haraka kwani mshtakiwa bado ni mgonjwa, lakini ofisi ya DPP nayo itoe kibali mapema ili mshtakiwa afahamu hatima yake kwa kuwa anateseka gerezani," alisema.

Akijibu madai ya wakili wa utetezi, Hakimu Salome, alikiri hati ya mashtaka inapaswa kurekebishwa na kuagiza upande wa Jamhuri kuifanyia marekebisho ili imtaje mshtakiwa Lengai Ole Sabaya pekee badala ya inavyosomeka sasa.

Hata hivyo, Hakimu Salome alisema DPP hawezi kuiendesha mahakama kama anavyotaka kama ilivyodaiwa na upande wa utetezi na badala yake inaendeshwa kwa mujibu wa sheria.

Awali katika maelezo yake mahakamani hapo, Wakili wa Jamhuri, Sabitina Mcharo, alidai mahakamani kwamba bado upelelezi wa shauri hilo haujakamilika, pia ofisi ya DPP haijatoa kibali kwa mahakama hiyo kusikiliza kesi hiyo.

Akijibu hoja za utetezi za sababu za kutoonekana kwa washtakiwa wanne, wakili Mcharo alisema Agosti 3, mwaka huu, washtakiwa Sylvester Nyegu, John Aweyo, Nathan Msuya na Antero Assey, waliingia makubaliano na DPP kisha kusomewa mashtaka mengine ambayo walikiri, kutiwa hatiani na kulipa faini.

Katika hati ya mashtaka baada ya kufanyika makubaliano, washtakiwa hao walisomewa mashtaka mawili, moja ni kujitwalia mamlaka na kufanya upekuzi kwa mfanyabiashara Alex Swai na la pili ni kula njama kushinda utaratibu wa haki.

Washtakiwa walikiri mashtaka hayo na hakimu Salome aliwataka kulipa faini ya Sh. 50,000 kila mmoja kwa kila kosa huku wakitakiwa kulipa fidia ya Shilingi milioni moja kwa Godbless Swai.

Mbali na kesi hiyo, mahakama hiyo iligeuka kuwa na vilio na kelele za watu wanaoaminika ndugu wa karibu wa Mshtakiwa Lengai Ole Sabaya wakipaza sauti za kuomba serikali kumsaidia kwa madai alikuwa mtumishi wa umma.

Septemba 6, mwaka huu mahakama ya hakimu mkazi iliwaachi huru washtakiwa wanne baada ya kusota mahabusu kwa siku 458, katika Gereza Kuu la Karanga Moshi, washtakiwa hao wamesota mahabusu kwa siku 95 na katika Gereza la Kisongo lililoko mkoani Arusha, walikaa kwa siku 363.

# Vituo vya afya vyashindwa kutoa huduma madai kukosa vifaa tiba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

VITUO vitatu vya afya vilivyojengwa kwa thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.5 katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama vimeshindwa kuanza kutoa huduma kwa kukosa vifaa tiba.

Hayo yaliyabainisha jana kwa nyakati tofauti na wananchi wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ikiwamo afya na elimu.

Mkazi wa Kata ya Kinaga, Agnes Mrisho, alisema wajawazito wanalazimika kutembea umbali mrefu wa kilometa 20 hadi Hospitali ya Mansipaa ya Kahama kupata huduma ya upasuaji na baadhi yao wanalazimika kujifungulia majumbani na njiani.

Alisema nauli ya kutoka kata hiyo mpaka hospitali ni Sh. 4,000, lakini nyakati za usiku wanatozwa Sh. 15,000.

Agnes alisema kama kituo kingeanza kutoa huduma kingekuwa mkombozi wao kwa kusaidia kuondoa shida ya vifo vitokanavyo na uzazi.

Diwani wa kata hiyo, Marry Manyambo, alisema awamu ya kwanza walipewa Sh. milioni 250 na kuanza ujenzi wa kituo cha afya na awamu ya pili walipokea Sh. milioni 250.

Kwa upande wake, Diwani wa Mwalugulu Halmashauri ya Msalala, Flora Sagasaga alisema wananchi wanalazimika kutembea umbali wa kilometa 30 hadi 40 kutafuta matibabu hususani kwa wajawazito.

"Mheshimiwa mkuu wetu wa wilaya kutoka hapa tulipo hadi Hospitali ya Manispaa ya Kahama ni umbali wa kilometa 40, wajawazito hawana budi kutembea umbali huo kunusuru maisha yao na watoto tumboni hivyo kukamilika kwa kituo hiki shida zote za uzazi zitakwisha," alisema Sagasaga.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Msalala, Erikana Zabroni alisema, halmashauri ilipokea Sh. milioni 537.5 kutoka serikali kuu kati ya hizo Sh. milioni 500 zilielekezwa kujenga kituo cha afya Mwalugulu na Sh. milioni 37.5 kukamilisha ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa Sekondari mpya ya Nyawile.

Alisema ujenzi umekamilika kwa asilimia kubwa ili kianze kutoa huduma na kwamba shida inayowakabili ni kukosekana kwa vifaa tiba hususani kwa wajawazito na watoto.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, alisema walipokea Shilingi bilioni mbili za kutekeleza miradi sita ya maendeleo ikiwamo ya afya na elimu.

Aliwataka wakurugenzi wa halmashauri hizo miradi hiyo inakamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma kwa wananchi kabla ya kumalizika mwezi Septemba, mwaka huu.



Rais Samia Suluhu Hassan akiangalia bidhaa katika mabanda ya maonesho kabla ya kuhutubia kwenye kongamano la Wanawake na Vijana wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) lililofanyika katika ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere (JNICC) Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Waomba polisi kuwakamata wanaoficha watoto wahalifu

**Na Rose Jacob,** MWANZA

BAADHI ya wananchi wa kata za Mabatini na Mbugani jijini hapo, wameliomba Jeshi la Polisi kuwakamata na kuwafanyia uchunguzi wazazi wanaowakumbatia watoto wao wanaojihusisha na vitendo vya kihalifu.

Wakizungumza katika mkutano wa hadhara ulioitishwa jana katika Viwanja vya Shule ya Pamba na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi mwishoni mwa wiki, baadhi ya wazazi walisema kuna watu wanakumbatia maovu katika jamii vikiwamo vitendo vya uhalifu.

"Tumechoka kuona amani inakosekana katika mitaa yetu, wanaotufanyia uvamizi, uhalifu na mauaji ni vijana wetu tunawafahamu, lakini wazazi wao wamekuwa mstari wa mbele kuwatetea," alisema.

Walisema hatua hiyo inalivunja moyo Jeshi la Polisi kulinda wananchi na mali zao.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Unguja, Michael Masongo, alisema katika eneo hilo hivi karibuni kijana Charles Chacha, alishambuliwa na vibaka kwa kuchomwa visu tumboni, lakini aliokolewa na kukimbizwa hospitali.

Akizungumza katika mkutano huo, Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, alitaka wananchi kushirikiana na viongozi wa kata hizo na polisi ili kuhakikisha wanaimarisha ulinzi na usalama.

"Hakuna tukio la kutumia bunduki, hawa ni vibaka wanajificha uchochoroni, ninawapa tahadhari wazazi mnaowaficha watoto wenu na kuwakumbatia ilhali mnajua ni wahalifu na wanahatarisha maisha ya watu na mali zao, mimi huwa sina mzaha ukinivuruga nitakuvuruga, lazima Mabatini kuwe na usalama na sio vinginevyo," alisisitiza Makilagi.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhan Ng'anzi, alikiri kutokea mauaji ya Yahaya Aboubakary ambaye alidaiwa kuwa kibaka.

"Licha ya historia mbaya ya marehemu kujihusisha na makundi ya uhalifu, lakini uchunguzi juu ya kifo chake unaendelea na kwa sasa hali ya usalama katika eneo hilo imezidi kuimarika na vijana wangu wako kazini kwa ajili ya kuhakikisha raia na mali zao wanakuwa salama bila kutishiwa na vibaka," alisema Ng'anzi.

# Uchakataji data za sensa wafikia hatua ya tatu

**Na Waandishi Wetu**

MTAKWIMU Mkuu wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS), Dk. Albina Chuwa, amesema wamefikia hatua ya tatu ya kuchakata data za sensa ili kupata taarifa itakayotolewa kwa umma.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu ushirikiano ulioanzishwa kati ya Ofisi ya Takwimu ya China na Tanzania kwa lengo la kuimarisha mifumo ya utoaji takwimu nchini, alisema uchakataji unaendelea vizuri.

Alisema hatua hiyo ni kusafisha data hizo na kwamba zitakamilika watapeleka kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye atazitangaza kwa Watanzania.

Dk. Chuwa alisema wameunda kamati ya ufundi kati ya wataalamu kutoka ofisi ya takwimu ya China na Tanzania kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kuona namna nzuri ya kuimarisha na kuboresha mifumo ya takwimu nchini.

"Wenzetu wameona kwamba wamesaidia kwenye maji, barabara na umeme sasa wameona kuna eneo la msingi la takwimu za nchi, hivyo wamekuja wanataka kuiunga mkono serikali katika kufanya ushirikiano wa pamoja, tuna mpango wa taifa wa kuimarisha na kuboresha takwimu, tumesha maliza awamu ya kwanza sasa tunaenda ya pili.

"Tutakuwa tunabadilisha uzoefu wa nchi ya China na Tanzania kama tunavyo shirikiana na nchi nyingine kama Sweden, Marekani na Norway, jambo la msingi tulilokubaliana na Balozi Chen Mingjian, ni kwamba tutengeneze mahitaji tuonyeshe nini hasa tunachokihitaji na mimi nimemwambia tutengeneze miundombinu ya takwimu," alisema.

Dk. Chuwa aliongeza kuwa malengo yao ni kufikia hatua ya kutoa takwimu kila baada ya robo mwaka na kwamba China ni kati ya nchi ambazo zimeendelea katika eneo hilo, akibainisha kwamba ushirikiano huo watoaufanyia kazi ili kulifanikisha hilo.

Pia alieleza kuwa kamati ya ufundi iliyoundwa kati cha China na Tanzania, itaangalia maeneo muhimu ya kusaidiana, ikiwamo kujenga uwezo wa mfumo mzima wa nchi kwenye wizara, idara na taasisi za serikali na katika serikali za mitaa ambako ndiko wanakwenda kuchukua data.

Vilevile, alieleza kuwa Serikali ya China imeridhishwa na namna Tanzania ilivyoendesha mchakato wa sensa na Serikali ya Tanzania ina mpango wa kutengeneza programu itakayotumika kutoa taarifa za takwimu kwenye simu.Balozi Chen alisema lengo la ushirikiano huo ni kuongeza uelewa kwa pande zote kwenye eneo la takwimu na wanashirikiana kwenye maeneo mengine ya uchumi, siasa na kijamii.

"Ushirikiano katika eneo la takwimu ni muhimu kwa nchi zote mbili, pia ni muhimu sana kujua idadi ya watu waliopo katika taifa na maendeleo yaliyopo katika sekta mbalimbali, pia takwimu zina umuhimu kwa serikali kwani zitasaidia kufanya uamuzi.

"Ninaamini mchakato wa sensa ulikwenda vizuri kwa manufaa ya maendeleo ya taifa na suala hilo limefanikiwa na tunapenda kushirikiana na Tanzania katika kulikamilisha hilo kwa kubadilishana uzoefu," alisema Chen.

***Imeandikwa na Maulid Mmbaga (DAR), Salma Twaha na Owen Bariki (TUDACo)**

## LATRA kuteta na Uber, Bolt

Na Maulid Mmbaga

MKURUGENZI Mkuu Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), Habibu Suluo, amesema wamefanya mazungumzo na Chama cha Madereva wa Teksi Mtandao Tanzania (TODA), Bolt na Uber ili kuangalia uwezekano wa kurudisha huduma hizo zilizositishwa awali.

Aprili 8, mwaka huu, LATRA ilitangaza viwango vya nauli za teksi mtandao na kampuni za mifumo ya teksi mtandao Bolt na Uber zilisitisha baadhi ya huduma za usafiri huo kutokana na kutoridhishwa na kiwango cha ukomo cha kamisheni cha asilimia 15 wanayopaswa kuwatoza madereva husika.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Arusha wakati alipokutana na wadau wa usafirishaji ili kujadili tiketi mtandao, alisema kati ya Septemba 5 hadi 8, mwaka huu, LATRA ilifanya vikao na TODA ili kutafuta suluhu ya changamoto inayoyakabili.

Alibainisha kuwa mazungumzo hayo pia yalihusisha kubadilishana taarifa na hoja za kibiashara na kiuchumi kwa lengo la kusaidia kampuni za mifumo ya teksi mtandao, madereva na abiria kupata huduma bora, endelevu na kwa thamani halisi ya pesa.

"Mazungumzo yetu baina ya TODA, Bolt na Uber yalikwenda vizuri, kuna taarifa ya maandishi tunasubiri tupate leo na si zaidi ya kesho toka kwa Bolt na Uber, ili tukamilishe taratibu zetu za ndani kabla hatujatangaza rasmi maamuzi ya mamlaka," alisema na kuongeza:

"Niwashukuru kipekee uongozi wa TODA na watoa huduma wa teksi mtandao walioendelea kutoa huduma ikiwa ni pamoja na Paisha, Ping, Indrive na Little Ride."

# Mambo matatu kutikisa Bunge

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO wa nane wa Bunge la 12, unaanza leo jijini hapo huku mambo matatu yanayotarajiwa kutikisa bungeni likiwamo sakata la tozo za miamala ya simu na benki.

Lingine ni uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) na kupitisha muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote.

Tozo imeendelea kuwa gumzo kwa wananchi licha ya serikali kuahidi kulishughulikia.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali inafanyia kazi hoja za wananchi kuhusu hilo na utekelezaji wake utatolewa hivi karibuni.

Kuhusu Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Rais Samia Suluhu Hassan juzi akihutubia katika Jubilee ya miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Umoja wa Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), alisema utapelekwa na kupitishwa bungeni mwezi huu kupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali namba mbili wa mwaka 2022.

Muswada wa Sheria ya Maafa 2022 pia utapelekwa kwenye mkutano huo.

Kadhalika, Bunge hilo litafanya uchaguzi wa wabunge wa EALA na Katibu wa Bunge ambaye ni Msimamizi wa Uchaguzi wa Wajumbe wa Bunge la Afrika Mashariki alitangaza uchaguzi wa wajumbe tisa watakaowakilisha Tanzania EALA utafanywa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa mkutano huo.

Uchaguzi huo unafanyika kwa kuzingatia kuwa maisha ya Bunge EALA lililoingia madarakani mwaka 2017, yatafikia ukomo wake Desemba 17, 2022.

Septemba 22, mwaka huu saa tano kamili asubuhi baada ya muda wa maswali, wakati Bunge linaendelea na shughuli zake utafanyika uchaguzi huo.

Vyama vya siasa ambavyo vimeonekana kuteua wajumbe wa kugombea nafasi hizo ni pamoja na Chama Cha Mapinduzi (CCM), ACT-Wazalendo na Chama cha Wananchi (CUF).



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akiongoza kikao cha kamati ya uongozi kilichopokea na kujadili shughuli za Mkutano wa Nane wa Bunge na mapendekezo ya ratiba ya mkutano huo jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kanuni biashara ya hewa ukaa mbioni kukamilika

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI inatarajia kutunga kanuni ya biashara ya hewa ukaa baada ya kuona fursa muhimu kwa wananchi waliohifadhi misitu kunufaika na rasilimali hiyo kwa kutunza mazingira.

Aidha, vijiji 10 vinanufaika na biashara hiyo huku halmashauri zikipata mapato ambayo yameboresha huduma za kijamii na kutoa bima ya afya kwa wananchi wanatunza mazingira.

Kutokana na biashara hiyo kwa mwaka 2021/22 vijiji hivyo vimepata zaidi ya Shilingi bilioni nne, ambazo ziligawanywa kwa vijiji na halmashauri kwa ajili ya huduma za kijamii, kutoa bima ya afya na kusomesha watoto.

Hayo yalibainishwa mwishoni mwa wiki na Ofisa Misitu Mkuu na Kiungo wa Mabadiliko ya Tabia Nchi wa Wizara ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Freddy Manyika, wakati akizungumza na waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (JET), katika mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili kuhusu mabadiliko ya tabia nchi na jitihada za kuhifadhi maeneo yaliyohifadhiwa.

Alisema vijiji vingi vinahifadhi maeneo yao kwa bidii kwa tumaini la kufanya biashara ya hewa ukaa kama wengine wanavyofanya, kutokana na hali hiyo serikali imeona ni muhimu kuweka utaratibu mapema.

Alisema fedha hizo hutolewa kama tuzo kwa waliohifadhi na kunyonya hewa ukaa kutoka angani na kwamba kuna vijiji vitatu eneo la Dareda-Karatu wanapata wastani wa Sh. milioni 200 hadi 500 kwa mwaka na vingine nane vipo Wilaya ya Tanganyika.

"Maombi ya vijiji kufanya biashara ya hewa ukaa yapo mengi, tumeona hatuna miongozo na kanuni hivyo tunakamilisha ili tuwe na utaratibu sahihi kwa nchi kunufaika na rasilimali hiyo, tayari tuna rasimu ya nyaraka hizo," alisema.

Naye Ofisa Wanyamapori Mkuu wa Idara ya Tawala za Mikoa, Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Hawa Mwechaga, alisema ajenda kuu ni kutunza rasilimali ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema hewa ukaa ni biashara mpya nchini na kwamba maeneo ya hifadhi ya jamii ya Makami, Kiteto wananchi wananufaika na vijiji vinane wilayani Tanganyika vinanufaika.

Hawa alizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi wa Idara ya Tawala za Mikoa, Beatrice Kimoleta, alisema wilaya ya Tanganyika eneo la hekta 216 limehifadhiwa kwa ajili ya kunyonya hewa ukaa na kwamba mwaka jana vijiji vilipata Sh. bilioni 1.3 na mwaka huu Sh. bilioni 2.1.

"Ukienda kwenye hivi vijiji wananchi wanajiona ni wamiliki wa mazingira wanawajibika kuyatunza, wamejenga shule, wanalipia watoto wao ada, hawana michango, wameajiri vijana 55 ambao amewasomesha Chuo cha Wanyamapori, Pasiansi Mwanza, kaya 5,000 zimepata bima ya afya na wanatarajia kuanzisha maduka mawili ya dawa," alibainisha na kuongeza:

"Kuna ujenzi wa shule unaendelea, vikundi vya wanawake vya vikoba vimepewa mikopo na mafunzo ya kuacha kuvuna raslimali misitu, pia kuna wafugaji nyuki zaidi ya 10,000 wanafuga kwa mizinga ya kisasa," alisema.

Kwa mujibu wa Hawa, Mfuko wa Misitu Tanzania ulio chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, ulitoa Sh. bilioni 2.3 ambazo zimejenga viwanda vya kusindika asali na kugawa mizinga ya kisasa inayodumu muda mrefu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo Rais kusikia kilio cha wananchi

**BAADA** ya kilio cha muda mrefu kuhusu tozo mbalimbali katika miamala ya kielektroniki hatimaye jana Waziri wa Fedha na Mipango, amesema amepokea maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Maelekezo hayo ni kushughulikia malalamiko ya wananchi yaliyojitokeza kuhusu gharama za tozo za miamala ya kielektroniki ili kuleta unafuu.

Kilio cha tozo kimewaibua wadau kutoka nyanja mbalimbali kuhusu mzigo wa tozo wanazotozwa wananchi na wengine hata kudiriki kutoa kauli za kukata tamaa ya kuhifadhi fedha katika benki kwa hofu ya tozo hizo.

Wengi wamekuwa wakihoji iweje mtu anapokwenda kuhifadhi fedha zake mahala salama, akatwe kodi na anapokwenda kuzitoa pia akatwe.

Wengine walikuwa wakilalamika wanapokwenda kulipa ushuru Mamlaka ya Mapato (TRA), pia anatakiwa aulipie tozo.

Hakika kilio kilikuwa kikubwa kuanzia kwa wananchi mmoja mmoja, mitandao ya kijamii na hata kwenye mikusanyiko ya watu.

Waziri wa Fedha Dk. Nchemba akiwa wilayani Tarime mkoani Mara katika ziara ya kikazi alitoa kauli hiyo ya kushughulikia kilio cha tozo wakati akizungumza na wananchi, wafanyabiashara na wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA.

Aliahidi kuwa wataalamu wa wizara yake wanayafanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na Rais, Chama Tawala (CCM) pamoja na maoni ya wananchi na kwamba muda si mrefu serikali itakuja na majawabu baada ya kufanya marekebisho ili kuleta unafuu.

Kwa wananchi tunasema hatua hii ni nzuri na inatia faraja kuona Rais wetu ni msikivu kwa kusikia kilio cha wananchi wake.

Watanzania wamejenga imani kwa Rais wao kwa kuwa wanajua ni msikivu ndiyo maana kilio cha tozo kilikuwa hakiishi midomoni mwao wakijua atasikiliza na amedhihirisha hilo kwa kuagiza lifanyiwe kazi.

Tozo huleta maendeleo katika nchi yoyote duniani, lakini ziangaliwe ili zisimuumize mwananchi ili naye aweze kufurahia anapoitoa akijua italeta faida.

Akifafanua kuhusu ukusanyaji wa mapato kwa ajili utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Waziri wa Fedha anasema unaenda sambamba na kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuweka miundombinu wezeshi inayolenga kuibua wajasiriamali wadogo, wa kati na wakubwa na hatimaye kuinua kipato cha mwananchi mmoja mmoja.

Pamoja na serikali kuhitaji fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali, lakini hata matumizi ya fedha hizo pia yaangaliwe kwa kuwa kilio kikubwa cha wananchi ni utumiaji unaozidi kiwango.


Wengi wanaolalamika wanadai matumizi makubwa serikalini kuanzia magari ya gharama ya viongozi na mambo mengine yanachangia kuleta malalamiko.

Hata baadhi ya miradi inayotekelezwa kuonesha kutumia fedha nyingi kuliko uhalisia wa mradi wenyewe.

Juzi tu Waziri Mkuu alipokuwa katika ziara, aligundua kibanda cha mlinzi na nyumba za watumishi wa umma kugharimu fedha nyingi katika ujenzi na kuamuru ufuatiliaji.

Mambo kama hayo huibua malalamiko na maswali kutoka kwa wananchi ambao hubeba mzigo wa kulipa tozo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Kuhujumu ujenzi wa vyuo VETA ni kuhujumu elimu

**MOJA** ya mikakati ya serikali katika elimu ni kufikisha kila wilaya Chuo cha Elimu ya Ufundi Stadi (VETA), ili vijana kuanzia shule ya msingi hadi wanaohitimu vyuoni wanapomaliza masomo wavitumie na kuwapa ujuzi.

Kutokana na mkakati huo takribani vyuo 43 vya VETA vimejengwa na vinafanya kazi na pia vipo 39 vinavyokamilishwa ili kwamba awe kijana wa darasa la saba au sekondari, akihitimu aandaliwe ili aweze kujitegemea.

Mkurugenzi wa Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dk. Noel Mbonde, anawashauri vijana kuona umuhimu wa kujiunga na vyuo hivyo.

Taasisi hizo ni ufunguo zinaweza kuwasaidia vijana kufunguka macho na kuachana na mtindo wa kutegemea kuajiriwa badala yake wajiajiri, hatua mbayo inaweza kupanua ajira zaidi kuliko ilivyo sasa ambapo wahitimu wamekuwa wakitegemea kupata kazi za maofisini pekee.

Lakini pamoja na mikakati hiyo ya serikali ya kutaka kuwapa vijana ujuzi kupitia vyuo hivyo, wapo baadhi ya watu ambao huenda wakaikwamisha na kusababisha washindwe kufanikisha kile ilichokusudia.

Kwa mfano, hivi karibuni Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alimuagiza Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Tabora, Musa Chaulo kuwakamata wote wanaohusika na usimamizi wa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha VETA Uyui kutokana na tuhuma za ubadhilifu wa fedha za mradi huo. Baada ya kuonyesha kutoridhika na gharama za ujenzi wa baadhi ya majengo, kikiwamo kibanda cha mlinzi.

Ilibainika kuwa ujenzi wa kibanda hicho umegharimu Shilingi milioni 11, na majengo yake kujengwa kwa gharama kubwa tofauti na uhalisia, huku pia akionyesha kutoridhishwa na nyumba za watumishi chuoni hapo zilizojengwa kwa kiwango kinachotia mashaka.

Nyumba moja ina uwezo wa kuchukua familia mbili, inajengwa kwa gharama ya Shilingi milioni 114 na tayari wameshatumia zaidi ya Sh. milioni 70, lakini bado ujenzi huo haijakamilika taarifa zinaeleza.

Kutokana na kutoridhishwa na ujenzi wa chuo hicho unaosimamiwa na VETA, Waziri Mkuu Majaliwa amemuagiza Mkuu wa Mkoa wa Tabora Balozi Dk. Batilda Burian, ausimamie ili kazi ikamilike kwa wakati.

Wakati umefika waliopewa dhamana kwenye miradi ya maendeleo ya umma watambue kushindwa kuisimamia ni sawa na kukwamisha maendeleo ya wanafunzi na nchi kwa ujumla kuwafedhehesha Watanzania.

Serikali inajenga vyuo hivyo, ili vijana waone umuhimu wa kujiunga, wasihangaike mitaani, kutokana na kwamba wakifika VETA, wanajifunza ujuzi wa aina yoyote wanaoupenda.

Zinapojitokeza tuhuma za aina hiyo katika ujenzi wa vyuo, ni wazi zinaweza kukwamisha mikakati ambayo serikali imejiwekea kwa ajili ya kupunguza wimbi la vijana mitaani, wasio na ajira.

Kwa mfano, Dk. Mbonde anasema serikali imetoa Sh. bilioni 100 kwa lengo la kutaka vijengwe vyuo vingine 36 vya wilaya, ili kufikia zaidi ya vyuo 100 ifikapo mwisho wa mwaka ya kesho.

Ninaamini kuwa VETA inakuza ujuzi na ubunifu wa vijana kwa ajili ya kuwasaidia kujiajiri na hata wengine kuajiriwa kwa urahisi kutokana na ubunifu wao, hivyo ninadhani si vizuri juhudi hizo za serikali kuhujumiwa.

Kimsingi, VETA inafungua fursa za ujuzi na ajira kwa vijana, hivyo ingependeza kama wale wanaotamani kujinufaisha kwa fedha zaa ujenzi wa vyuo hivyo wataachana na tamaa hiyo na kusimamia ujenzi inavyotakiwa.

Mahitaji ya kupata ujuzi kwa Watanzania, hasa vijana kuwa makubwa huku yakizidi kuongezeka kila uchao, ninadhani ndio sababu ya kuifanya kuja na mkakati wa kuwa na chuo kila wilaya.

Hivyo, ingekuwa vyema iwapo wale wanaotamani kufanya hujuma wakajiweka pembeni, ili lengo la serikali la kutaka kuwapa ujuzi vijana wa Kitanzania na kuwawezesha kujiajiri liweze kutimia.

# Serikali yapewa angalizo Bima ya Afya kwa Wote

**Na Elizabeth Zaya**

SIKU moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutamka Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambao utawasilishwa wakati wa mkutano wa Bunge unaoanza leo, wadau wa afya wameishauri serikali mambo ya kuzingatia ili huduma hiyo iwe nzuri na endelevu.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, wadau hao walisema ni muhimu serikali kujipanga na kuweka mifumo ya kudhibiti mianya ya ubadhirifu na kuzuia fedha za bima hiyo kutumiwa kutekeleza miradi mingine ya maendeleo.

Waziri wa zamani wa Mambo ya Ndani na Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwanga alisema mipango ya serikali kuanzisha bima ni jambo jema, lakini akashauri kuwe na mfumo maalum wa kidijitali utakaodhibiti ubadhirifu wa fedha.

"Ni mpango mzuri sana ambao serikali inakuja nao, kikubwa ni kuangalia namna ya kuusimamia na kuuwezesha. Wasiwekwe watu ambao ni wababaishaji.

"Na ni vizuri endapo ukianza kuwe na mfumo maalum wa kidijitali utakaosaidia kudhibiti ubadhirifu wa aina yoyote, kila kitu kiendeshwe kidijitali, ili kila kitu kinachofanyika kiwe kinaonekana kwa urahisi. Na pia ufuatiliaji wake uwe mkubwa na wa karibu," Kitwanga alishauri.

Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Kijo Bisimba, alisema bima hiyo ikianzishwa, mfuko unaosimamia usiingiliwe na serikali kwa kuchukua fedha na kuzipeleka kwenye matumizi mingine.

Alishauri kuwe na mamlaka ya usimamizi wa mfuko huo ambayo haitaingiliwa, bali kuhojiwa na mamlaka kubwa ili kulinda fedha zake kuchukuliwa na kushindwa kufikia lengo la kutoa huduma bora.

"Ni muhimu jambo hili la Bima ya Afya kwa Wote lichukuliwe kwa umuhimu wake. Isiingiliwe na serikali, mamlaka yake iwe yake tu na fedha yake isichukuliwe kufanyia vitu vingine, hata zikijaa ziachwe tu.

"Iwekewe mfumo mzuri wa kudhibiti ubadhirifu, wizi na udanganyifu na fedha isitumike vibaya. Watumishi wasio waaminifu wawekewe mfumo mzuri wa kuwadhibiti," alisema.

Mwanaharakati na mchambuzi wa masuala ya kisiasa nchini, Deusi Kibamba, alishauri bima hiyo kuelekezwa kwenye matibabu pekee ili kila Mtanzania apate huduma bora za afya.

"Hili ni jambo jema sana na ni mapendekezo yangu kwamba ianze na matibabu ya afya tu kwanza, isianze na mambo mengi, hayo mengine yatafanyika huko kwingine.

"Na pia taasisi mbalimbali za serikali ziuchangie mfuko ili ukahudumie vizuri wananchi. Ila kwa ujumla hili ni jambo jema sana, kilikuwa ni kilio cha Watanzania muda mrefu," alipongeza.

Juzi akihutubia kwenye maadhimisho ya Jubilei ya Miaka 50 ya Chama cha Kitume cha Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), Rais Samia alitangaza muswada huo uliosubiriwa kwa muda mrefu, utapitiwa na kupitishwa katika mkutano huo wa Bunge unaoanza leo jijini Dodoma.



Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde (kushoto), akimkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, tuzo ya usimamizi mzuri na ubora wa zao la korosho katika msimu wa 2021/2022 kwenye hafla iliyofanyika mjini Songea na kushirikisha wadau wa zao la korosho kutoka mikoa 17 nchini. **PICHA: GIDEON MWAKA NOSYA**

## Yashauriwa kuwajengea uwezo wakulima

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI imeombwa kuwajengea uwezo wakulima ili waandae, watunze na kutumia vizuri pembejeo za kilimo, ili kufikia malengo ya ajenda 10/30 (kilimo kukua kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030).

Kadhalika, serikali imeweka malengo ya kuhakikisha kilimo kinakuwa kwa asilimia hiyo ifikapo mwaka 2030, baada ya sasa kukua kwa asilimia 5.7.

Akizungumza na gazeti hili, Mratibu wa kitaifa wa mtandao wa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayohamasisha utunzaji wa baionuai ya kilimo (TABIO), Abdullah Mkindi, alisema ili kufikia malengo ya ajenda hiyo ni lazima wakulima wapatiwe uwezo wa kuzalisha na kutunza mbegu, uandaaji na utunzaji wa mbolea ya asili.

"Kwa sasa zaidi ya asilimia 70 ya mbegu zinazotumika na wakulima ni zile zilizohifadhiwa kutoka msimu mmoja kwenda msimu mwingine, pia bado wakulima kwa kiasi kikubwa wanatumia mbolea za asili kurutubisha mazao yao," alisema na kuongeza:

"Bado kuna changamoto ya namna ya uandaaji wa mbegu pia matumizi sahihi ya mbolea na viuatilifu, hapa ndipo tunasema serikali sasa kupitia wizara husika inapaswa kuwajengea uwezo wa kuandaa hizo mbegu, mbolea na viuatilifu si kuandaa tu pia matumizi yake na utunzaji."

Alisema, licha ya wakulima kutumia viuatilifu kukabili wadudu waharibifu wa mazao, bado kuna changamoto ya namna ya kuviandaa, utunzaji na kiwango kinachotumika ili kuepuka madhara.

"Hizi ni dawa za asili kuna dozi inayotakiwa kutumika kwenye mmea, hapa watu wa taasisi ya utafiti wa kilimo (TARI) wanaweza kusaidia kufanya utafiti wa namna ya kuandaa, utunzaji wake, pia dozi inayotakiwa kutumiwa," alisema Mkindi.

Aidha, alisema halmashauri zinapaswa kutoa vifaa vya kuchakata mbolea na kuandaa viuatilifu kwa wakulima kuwasaidia kuboreshwa kilimo.

"Wote tunafahamu malengo endelevu ya milenia yanaweka wazi 'hakuna anayeachwa nyuma', kama tunataka kuongeza tija kwenye kilimo ni lazima tuwaangalie wakulima wadogo ambao zaidi ya asilimia 80 wanatumia mbegu zao wenyewe, bila kufanya hivi tunaweza tusifikie malengo yaliyowekwa," alibainisha Mkindi.

## Mpango awageukia wenyeviti na mameya utekelezaji miradi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amewataka wenyeviti wa halmashauri na mameya wa majiji, kusimamia vizuri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyotakiwa.

Amewataka kuepuka vitendo vya rushwa na ufujaji wa fedha za miradi ili wananchi wapate huduma bora na waone matokeo ya fedha za kodi wanazozitoa kwa serikali yao.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini hapo alipozindua Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa (ALAT) ambao unafanyika kwa siku nne na kushirikisha wenyeviti wa halmashauri zote za wilaya, miji na mameya wa majiji yote nchini.

Alisema serikali imekuwa ikitekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo nchini ikiwamo sekta za afya, elimu na barabara kwenye halmashauri zote nchini kwa kutumia fedha zinazotokana na vyanzo mbalimbali.

Alisema tatizo lililopo ni baadhi ya wasimamizi wa miradi hiyo kutokuwa waaminifu kwa kuzichepusha fedha hizo na kuzitumia kwa maslahi yao binafsi hali ambayo inafifisha juhudi za wananchi kupata huduma bora.

"Kinachosikitisha ni kwamba kwenye halmashauri zetu bado kuna mchwa wanaotafuna fedha, fedha zinatengwa kwa ajili ya miradi, lakini wao wanazichepusha na kuziingiza kwenye mifuko yao binafsi, nawaombeni sana ninyi mlioaminiwa fanyeni kazi kwa uadilifu," alisema Dk. Mpango.

Alisema yeye ni miongoni mwa viongozi wanaotafsiriwa kwamba ni wapole, lakini huwa sio mvumilivu kwa kiongozi yeyote anayefuja mali za umma na kusisitiza kuwa watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Alisema Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) iliyoishia Juni 30, 2021 ilionyesha kuwa baadhi ya halmashauri zilipata hati chafu na asilimia 17 ya halmashauri zilishindwa kurekebisha kasoro ama kujibu hoja za ukaguzi.

"Pia ripoti hiyo ya CAG ilionyesha kuwa kulikuwa na dosari kwenye manunuzi ikiwamo manunuzi yaliyofanyika bila ushauri wa Bodi za Wazabuni, ununuzi ambao haukufuata utaratibu wa kushindanisha wazabuni na fedha kutorejeshwa na makandarasi baada ya mikataba kuvunjika," alisema Dk. Mpango.

Mwenyekiti wa ALAT Taifa, Murshid Ngeze, alisema lengo la jumuiya hiyo kwa mwaka huu ni kuongeza ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri na majiji pamoja na kusimamia matumizi ya mapato hayo kwenye utekelezaji wa miradi.

Alisema mamlaka za Serikali za Mitaa zinafanya kazi nzuri, lakini zinakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo malipo kidogo kwa madiwani na wakurugenzi hali ambayo alisema wakati mwingine huwa inawavunja moyo.

Ngeze alisema maboresho ya mwisho ya stahiki za madiwani yalifanyika mwaka 2014 na kwamba hayajafanyika mabadiliko mengine mpaka sasa hali aliyosema haiendani na hali ya maisha ya sasa.

"Wakurugenzi wa halmashauri zetu wanafanya kazi nzuri sana lakini kwa sababu wao ni waajiriwa wa serikali huwa hawawezi kusema, sisi ndiyo wasemaji wao kwa hiyo tunaomba waboreshewe maslahi yao," alisema Ngeze.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alizishukuru halmashauri kwa kuendelea kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Alisema katika mwaka wa fedha uliopita halmashauri zilikusanya zaidi ya Sh. bilioni 800 lakini matarajio ni kufikisha zaidi ya Shilingi trilioni moja kutokana na kuongezeka kwa vyanzo vya mapato.

# Serikali yafanya tathmini uhai wa shoroba nchini

**Na Salome Kitomari, aliyekuwa**
DODOMA

SERIKALI imesema imepitia shoroba zote nchini na kufanya tathmini ya zinazohitajika kufufuliwa ili wanyama waendelee kupita na ambazo hazifai kwa matumizi kutokana na kukithiri kwa shughuli za kibinadamu.

Vilevile, imesema ripoti ya hali ya shoroba hizo na mpango kazi zitawekwa hadharani Jumamosi ya wiki hii jijini Dodoma, kwenye kikao kitakachowaleta pamoja wadau wa uhifadhi nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari waliofanya mahojiano na viongozi mbalimbali wa sekta zinazotegemeana kwenye uhifadhi na utalii, Mkurugenzi wa Wanyamapori Tanzania, Dk. Maurus Msuha, alisema kuna shoroba zimefungwa kabisa haziwezi kufufuliwa, zenye afadhili zinahitajika kuokolewa na ambazo ziko vizuri wanyamapori wanapita bila kikwazo.

Waandishi hao ambao ni wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), kupitia mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, walifanya ziara hiyo kwa ajili ya kukusanya taarifa za kuelimisha umma.

Alisema: "Kwa kutambua umuhimu wa shoroba, tunashirikiana na wadau kuwaomba wananchi waridhie kufanya mpango wa matumizi bora ya ardhi, ili shughuli zinazofanyika zizingatie umuhimu wa wanyama kupita bila kizuizi.

"Ninafananisha shoroba na mkondo wa mto, ukiziba unatengeneza mafuriko na ndiyo maana kelele nyingi sana lazima tukubali maeneo mengi ambayo wanyama wangepita yamezibwa, ukiwazuia wasipite, lazima unatengeneza mgogoro, suluhisho pekee ni kutafuta namna ya wao kupita."

Mkurugenzi huyo alisema maeneo hayo yatatambuliwa rasmi na wananchi wakiridhia utaratibu huo, Waziri wa Maliasili na Utalii atatangaza kwenye gazeti la serikali na kutakuwa na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Dk. Msuha, alisema serikali imeanza mchakato wa kuzitambua na zingine zinafanyiwa tathmini kuona kama zinapitika na kuendelea kuzihifadhi na kwamba ripoti hiyo imeweka mpango kazi wa kutunza maeneo hayo.

"Uhalisia maeneo ya shoroba hayawezi kubaki kama kisiwa, wanyama kama tembo wanahitaji maeneo makubwa ili kupata mahitaji yao, lazima watoke kwa ajili ya mahitaji na kubadilishana vinasaba ili wasiendelee kuzaliana wanyama wa aina moja (ndugu), ni muhimu kubadilishana vinasaba ili kulinda kuwapo kwao," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, shoroba siyo mali ya serikali, bali nje ya hifadhi na kwamba kutokana na ongezeko la watu, shughuli za kibinadamu nazo zimeongezeka.

"Ushoroba wa Kwakuchinja, Babati ukifa, utakuwa ndiyo mwisho wa Hifadhi ya Taifa Tarangire na Ziwa Manyara kwa sababu ndicho kiunganishi... miaka ya nyuma ulikuwa unapitika lakini kwa sasa mapito ya wanyama yaliyobakia ni njia tatu pekee, jambo linaloongeza migogoro," alisema.

Aliongeza kuwa migogoro baina ya wanyama na binadamu imeanza kuongelewa hivi karibuni kuliko miaka 30 iliyopita kutokana na kuongezeka kwa watu huku ardhi ikiwa ileile, pia mahitaji ya rasilimali hiyo kwa ajili ya kilimo na matumizi mingine ya kibinadamu yanazidi kuongezeka.

"Njia tunayotumia kuhakikisha rasilimali ya wanyamapori inahifadhiwa ni kutenga maeneo ya hifadhi kwa kufanya tathimini wa eneo husika kabla ya kuhifadhiwa pamoja na kuhifadhi haimaanishi mahitaji yote ya wanyamapori muhimu yanapatikana kwenye eneo husika.

"Mfano, Hifadhi ya Taifa Tarangire imeanzishwa kisheria, haimaanishi kwamba wanyamapori maisha yao yote yatakuwa ndani ya hifadhi, kuna mahitaji mengine hayapatikani ndiyo maana kuna kipindi wanyama wanatoka nje ya hifadhi kupata mahitaji, unapoanzisha hifadhi inawezekana usiguse mahitaji yote.

"Kipindi cha masika Tarangire kwa miezi sita kunakuwa na majani marefu sana ambayo kwa wanyama wenye mimba ili walee watoto vizuri, lazima watoke nje kwenda eneo la mtawanyiko la Simanjiro ambalo lina majani mafupi ambayo yana virutubisho vizuri kuliko marefu, hivyo ni muhimu kwa wanaonyonyesha, pia wanahitaji chumvi na udongo," alisema Dk. Msuha.

Alisema, utekelezaji wa kutunza shoroba unafanyika kwa ushirikiano na sekta nyingine kama serikali za mitaa, ardhi na mifugo na wameshirikiana kwa kiasi kikubwa.

Mkurugenzi Mtafiti wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Joseph Paul, alisema ni muhimu ardhi ikapimwa ili kuondoa migogoro, akiwa na ufafanuzi kwamba maeneo yaliyopimwa, yana mafanikio makubwa na wananchi wananufaika na rasilimali za uhifadhi.

"Ili tupime eneo la kijiji na kuja na mpango wa matumizi bora ya ardhi, tunahakikisha ni hitaji liliibuliwa na kuridhiwa na wananchi wenyewe, tunazingatia ukubwa wa kijiji, umbali na upitikaji wa miundombinu, mwinuko wa ardhi. Baadhi ya maeneo wameona umuhimu na wengine hawajaona,"alisema.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akizindua Mwongozo wa Kitaifa wa Uanzishaji na Uendeshaji Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi wilayani Kibaha mkoani Pwani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania kuwa kitovu cha mawasiliano Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, amesema Tanzania itakuwa kitovu cha maunganisho ya mawasiliano Afrika Mashariki na Kati kufuatia kuwapo mkongo wa pili wa Afrika.

Pia, amesema mkongo huo wa pili Africa Submarine, unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2023 kwa kufika katika zaidi ya maeneo 35 katika nchi 26 duniani.

Alibainisha hayo jana wakati wa ziara ya kukagua mkongo wa kituo cha pili Afrika kinachojengwa Dar es Salaam na kampuni ya mawasiliano ya simu ya Airtel kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za serikali kuifanya Tanzania kitovu cha maunganisho ya mawasiliano.

Alisema, kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho, kuna faida kubwa kwa nchi kupata mtandao wa intaneti wenye kasi zaidi na uhakika wa kuunganishwa duniani.

"Mkongo unaokuja unapitia kusini mwa Bara la Afrika. Kwa hiyo, tutapata uhakika wa maunganisho kwenda duniani na kusaidia sana biashara ya kuuza 'capacity' (uwezo) nchini mwetu na nchi jirani na kuwasaidia wenzetu kushiriki uchumi wa kidigitali ambao ndiyo uchumi wa dunia," alisema.

Mkurugenzi wa Masuala ya Udhibiti na Mawasiliano, Beatrice Singano, akizungumza kwa niba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel, alisema wanatengeneza eneo la kusambaza mawasiliano yanayopitia baharini (Sea Cable Services), ili kuiwezesha Tanzania kufikiwa na kufikia maeneo mengine kimawasiliano.

Alibainisha mkongo huo unatoka Djibouti, na unahimili kwa kiwango kikubwa kutoa mawasiliano pamoja na kuiwezesha Tanzania kukua kimawasiliano, huduma hiyo pia ikizinufaisha nchi jirani.

"Mkongo huo mpya wa kisasa utakaotoa mawasiliano ya kasi ya hali ya juu kiasi cha terabytes 180 ni mmoja kati ya mikongo mikubwa duniani utakaotokea Bara la Ulaya na kukatiza mashariki ya kati kwa kupitia nchi mbalimbali za Afrika hadi nchini," alisema.

## Waliokimbia enzi za Mrema waitwa

**Na Sabato Kasika**

UONGOZI wa Tanzania Labour Party (TLP), umewataka wanachama wa chama hicho waliokihama kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo za kutoridhishwa na uongozi, kurejea kundini.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Richard Lyimo, alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozungumzia mikakati ya kuimarisha TLP baada ya kifo cha Mwenyekiti wa Taifa, Augustine Mrema.

"Ninawaomba wanachama wote wa TLP, ambao waliondoka katika chama kwa kukwazwa au kutoridhishwa na uongozi, warudi ili tukijenge chama chetu kiwe kwenye hadhi kama ilivyokuwa miaka ya nyuma," alisema Lyimo.

Katibu Mkuu huyo alisema kwa nyakati tofauti chama hicho kimekimbiwa na baadhi ya wanachama wake wakiwamo wenye majina makubwa ambao sasa anawataka warudi kukijenga.

"Hatuna masharti yoyote kwao, ila jambo la msingi ni kwamba tunawaomba warudi katika chama chao tukijenge kwa pamoja ili tujiandae kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025," alisema.

Lyimo alisema kuwa baada ya TLP kupatwa na msiba wa kuondokewa na mwenyekiti wake, hawana budi kujipanga upya ili kuhakikisha chama kinaendelea na harakati za kisiasa kama kawaida.

Alisema wameanza kwa kupata Kaimu Mwenyekiti wa TLP Taifa, Alhaji Hamad Mkadam, aliyechaguliwa na sekreterieti ya chama wiki iliyopita.

"Baada ya kupata Kaimu Mwenyekiti, sasa tunaelekeza nguvu zetu katika kurejesha wanachama pia kutafuta wafadhili wa kutupa fedha za kukarabati jengo letu lililochakaa," alisema.

Aliongeza kuwa kiongozi aliyepita alikuwa na mikakati yake na sasa chama kiko chini ya uongozi mwingine wenye mikakati mingine ambayo lengo lake ni kuhakikisha TLP inarudi kwenye chati.

"Ninaamini hilo linawezekana, ndiyo maana ninawaomba wanachama wetu wote waliohamia katika vyama vingine na wengine kubaki bila chama, warudi tuungane kujenga chama chetu," alisema.

Aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Hamad Tao, alipoulizwa kuhusu wito huo wa TLP, alisema yuko tayari kurejea lakini akataka aelewane na uongozi kwanza kwa mambo yanayohusu kufanya shughuli za kisiasa.

"Kuna watu pale wanang'ania madaraka bila kufanya kazi, mimi si mtu wa kula kulala, hivyo kama watanitaka nirudi, basi wakubali nifanye mikutano ya hadhara kuingiza wanachama wapya, vinginevyo inakuwa vigumu kurudi, kwa sababu mimi ni mtu wa kazi," alisema Tao.

# Kampeni: 'Ukimwona mtoto wa shule kimbia usimsogelee'

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, amemwagiza Ofisa Elimu mkoani humo, Dafroza Ndalichako, kuanzisha kampeni maalumu ya 'Ukimwona mtoto wa shule kimbia usimsogelee' ili kukabiliana na tatizo la mimba na ndoa za utotoni.

Mkoa wa Shinyanga unakabiliwa na tatizo la wanafunzi kubebeshwa ujauzito na wengine kuozeshwa ndoa za utotoni na kuzima ndoto zao za masomo.

Mjema alitoa agizo hilo kwenye uzinduzi wa vitabu vya mkakati wa kuboresha elimu nchini, mkoani humo na kukemea vitendo vya wanafunzi kuendelea kukatishwa masomo yao kutokana na ujauzito na ndoa za utotoni.

"Serikali chini ya Rais Samia imekuwa ikiboresha miundombinu ya elimu ili watoto wetu wasome na kutimiza ndoto zao kwa kuwa taifa linawategemea, lakini hapa Shinyanga bado kuna tabia ya kubebesha mimba wanafunzi na kuwaozesha ndoa za utotoni nalo tunalitafutia dawa," alisema Mjema.

"Mimba na ndoa zipo hasa kwa wanafunzi ambao wanahitimu darasa la saba, wakiwa huko majumbani mwao wakisubiri matokeo yao ndipo hufanyiwa vitendo hivyo nakuagiza ofisa elimu mkoa kuanzisha kampeni maalumu 'ukimwona mtoto wa shule kimbia usimsogelee, mshirikiane na dawati la polisi," aliongeza. Aidha, alikemea vitendo vya wazazi mkoani humo kumalizana kienyeji na watuhumiwa kimya kimya ambao huwapatia ujauzito mabinti zao na kuamua kuacha kutoa ushahidi mahakamani.

Alisema hatua hiyo inachangia kuongezeka kwa mimba na ndoa za utotoni kwa kuwa watuhumiwa wanajua wakitenda kosa hilo watamalizana na wazazi wa msichana.

Katika hatua nyingine aliwataka wazazi mkoani humo, kuzuia matumizi mabaya ya mitandao ya simu kwa watoto wao, pamoja na kujiunga kwenye vikundi vya Whatsapp ili kuwaepusha kujifunza tabia mbaya na kusababisha mmomonyoko wa maadili.

Kwa upande wake, Ndalichako alisema vitabu hivyo vya mkakati wa kuboresha elimu nchini, vitasaidia kukuza elimu mkoani humo.

Alisema licha ya kuanzisha mkakati huo, watakuwa wanakaa vikao na wazazi na kuzungumzia masuala ya elimu.




Jengo la Makao Makuu ya Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), Magomeni Usalama Dar es Salaam likiwa katika hali mbaya. Katibu Mkuu wa chama hicho, Richard Lyimo amewaomba wanachama na wafadhili wakisaidie fedha chama ili walikarabati jengo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Ruvuma ina ziada chakula zaidi tani 700,000

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKOA wa Ruvuma una kiwango cha utoshelevu wa chakula kwa zaidi ya miaka 12 mfululizo.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas, ameyataja mahitaji ya chakula mkoani humo kwa msimu wa mwaka 2022/2023 ni tani 469,172 na kuufanya kuwa na ziada ya chakula tani 787,190.

Kadhalika, alisema chakula kilichozalishwa katika msimu wa mwaka 2021/2022 kinatumika msimu huu wa mwaka 2022/2023 na katika mazao ya chakula zilizalishwa tani 1,256,362.

"Mkoa wa Ruvuma ni mzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula na biashara, kwa miaka minne mfululizo umeendelea kwa kuongoza kitaifa katika uzalishaji wa chakula nchini," alisema.

Akizungumzia mazao ya biashara, aliyataja mazao ya kimkakati yanayowaingizia wakulima kipato kuwa ni zao la kahawa ambalo kwa msimu wa mwaka 2021/2022 jumla ya kilo milioni 13.7 ziliuzwa na kuingiza Sh. bilioni 97.

Mazao mengine ya kimkakati ameyataja kuwa ni ufuta ambalo katika msimu uliopita limewaingizia wakulima Sh. bilioni 23.4, soya Shilingi bilioni sita na mbaazi Sh. bilioni 1.3.

Alisema katika msimu ujao wa kilimo mkoa huo unahitaji mbolea tani 50,280 na sasa usajili wa wakulima kwa ajili ya mbolea ya ruzuku unaendelea ukiwa umesajili wakulima 216,366.

# Waandishi wa habari wahakikishiwa usalama kazini

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Albert Msando amewataka waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa kufuata sheria, taratibu na weledi na kuahidi kuwa hakuna atakaye nyanyaswa na kunyang'anywa vitendea kazi vyake katika majukumu yake ndani ya wilaya hiyo.

"Fanyeni kazi yenu kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo, hakuna wa kukunyanyasa, wala kukupora camera yako au simu au kitendea kazi chochote kile awe Polisi au Magereza katika Wilaya ya Morogoro, akifanya hivyo nipeni taarifa mapema," alisema Msando.

Alitoa kauli hiyo katika mdahalo ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Morogoro (MORO PC), wenye dhima ya kulinda usalama wa mwandishi wa habari akiwa kazini ulioandaliwa na kufadhiliwa na Shirika la Ims na kusimamiwa na Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

Alisema, waandishi wa habari watalindwa na kuwezeshwa kufanyakazi zao kwa ufasaha na kuendelezwa kiuchumi ili waweze kuendana na hali halisi ya kimaisha. Alisema Rais Samia Suluhu Hassan, ameonyesha njia ya serikali yake kufanya kazi zake kwa uwazi na kwamba hakuna sababu ya kuwakwepa au kuficha taarifa kwa waandishi wa habari bali ni kuwapa ushirikiano waweze kutimiza majukumu yao.

Mkuu huyo aliziagiza taasisi za serikali zilizopo wilayani humo kuacha urasimu wa utoaji habari kwa waandishi wa habari kwa kuwa wapo kwa mujibu wa Katiba na mikataba ya kimataifa katika kutekeleza majukumu hao.

"Katika wilaya yangu sitaki kusikia kuna taasisi inanyima taarifa waandishi wa habari kwa kisingizio eti hakuna msemaji, lazima muwape taarifa na ushirikiano wa kutosha waandishi wa habari," alisema Masando.

Alizitaka taasisi hizo kutenga bajeti za kuwezesha waandishi wa habari kushiriki kikamilifu katika matukio mbalimbali ndani ya wilaya hiyo ili wawajibike ipasavyo kuhabarisha umma utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya kitaifa ya kimkakati.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Moro PC, Nickson Mkilanya, aliziomba mamlaka za serikali mkoani humo kuwalinda na kuwapa ushirikiano waandishi wa habari ili waweze kuhabarisha umma kwa kuwa hiyo ni haki ya kikatiba.

Alisema, waandishi wa mkoa huo wanafanya kazi kubwa ya kuelimisha jamii, lakini zipo baadhi ya taasisi zinashindwa kutoa ushirikiano kwa kutumia kigezo cha kutokuwapo kwa wasemaji.

Baadhii ya waandishi wa habari waandamizi, akiwamo Idda Mushi na Aziz Msuya, walisema ni budi kwa vyombo vya ulinzi na usalama kuwalinda waandishi wa habari kwa vile wanasaidia kusukuma maendeleo ya taifa.

Walitoa rai, kwa wanatasaluma wenzao kutoutumia uhuru wa habari vibaya kwa kufuata sheria na kuzingatia taratibu na maadili ya uandishi wa habari.

# Waagizwa kufunga CCTV kamera maghala korosho kuimarisha ulinzi

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

BODI ya usimamizi wa stakabadhi ghalani imewaagiza waendesha maghala wote ya korosho nchini kufunga teknolojia ya CCTV kamera kwenye maghala yao ili kuwezesha ufuatiliaji wa karibu mwenendo wa shughuli zinazofanywa pamoja na kuimarisha ulinzi.

Hatua hiyo inatokana na malalamiko ya mara kwa mara kwa baadhi ya waendesha maghala ambao wamedai kupokea korosho zenye ubora hafifu na kutoa taarifa zisizo sahihi katika mchanganuo wa mauzo hali inayosababisha migogoro na wanunuzi pamoja na wadau wa zao hilo.

Akizungumza na gazeti hili jana mkoani hapo, Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi hiyo, Asangye Bangu, alisema kutokana na changamoto zinazolalamikiwa na wadau wa zao hilo wameona umuhimu wa kuwekwa kwa teknolojia hiyo kwenye maghala yote.

Bangu alisema kama maghala yote yatafungwa kamera hizo itasaidia ufuatiliaji mzuri wa shughuli zinazofanywa moja kwa moja na malalamiko hayatakuwapo.

Alisema ofisi yake itapata taarifa zote na kwa urahisi zaidi. "Tayari tumeshaandaa ofisi na sehemu ambayo tutakuwa tunaunganisha kwenye mtandao waendesha maghala wote ambao tayari tumeshawapa leseni kwa sababu sasa hivi wameshakuwa kwenye mtandao hivyo tutawaunganisha ili waje kutoa taarifa ya nini kinachoendelea kwenye maghala yao," alisema Bangu.

Alisema teknolojia hiyo pia itawezesha kuongeza utendaji kazi ambao utakuwa wa ufanisi zaidi kwa sababu taarifa zote zitakuwa zikitolewa kwa usahihi na ubora unaotakiwa na kufanya wadau kuamini kile kinachotolewa kwenye zao la korosho.

Bangu alisema agizo hilo linapaswa kutekelezwa haraka iwezekanvyo ili kuanzia msimu huu wa zao la korosho kila ghala liwe na teknolojia hiyo.

Mkurugenzi alisema bodi itachukua hatua kali za kisheria kwa watakao kwenda kinyume na taratibu na sheria na kuwaonya wanaojihusisha na ubadhirifu wa korosho.




Mkazi wa Kipunguni, Happy Luambano (kulia), akiwa katika mafunzo ya jinsi ya kusimama jukwaani na kuomba kura juzi, ambayo yanaendeshwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujengea wanawake uwezo wa kushiriki katika uchaguzi ili waweze kuongezeka katika ngazi za maamuzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wadau wapendekeza bajeti kuzingatia usawa kijinsia

**Na Yasmine Protace**

WADAU wa masuala ya Semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS), wamependekeza kuwapo umuhimu wa bajeti inayotekeleza na kuzingatia usawa wa kijinsia.

Washiriki wa semina hiyo iliyoratibiwa na TGNP Mtandao, walichangia hayo katika mada iliyokuwa ikizungumzia uwezeshaji wa wanawake kupitia bajeti yenye mrengo wa kijinsia.

Mwanaharakati wa masuala ya kijamii, Juma Ally, alisema umuhimu wa kuwa na bajeti yenye mrengo wa kijinsia unasaidia kuwaondolea kero wananchi katika makundi yote maalum.

"Kutozingatia masuala ya mrengo wa kijinsia husababisha kero katika huduma za kijamii zikiwamo za afya, maji na nyingine nyingi," alisema.

Hamida Jamal, kwa upande wake alisema kuwa bajeti yenye mrengo wa kijinsia inazingatia upatikanaji wa fedha mgawanyo na mahitaji yaliyopo na nani yanamgusa, zaidi jamii inahitaji afya, shule, maji na huduma nyingine muhimu.

Alisema katika huduma hizo mahitaji ya wanawake ni mengi zaidi kuliko wanaume na kwamba bajeti ikizingatia mahitaji ya wengi itakuwa rahisi kupunguza kero zinazowakabili wanawake.

"Kwa mfano katika shule wanafunzi wa kike wanatakiwa kuwa na matundu ya vyoo ya kutosha, chumba cha kujihifadhi, kuwe na taulo za kike na maji ya uhakika katika shule," alisema.

Idd Mziray, anayetoka katika Shirika la Jinsia na ujana, alisema nchi inataja bajeti kila mwaka, lakini bado kwa upande wa wanawake kumekuwa na changamoto kunufaika kupitia bajeti hizo.

"Ukiangalia bajeti ya kilimo imeongezwa kiasi kikubwa cha fedha, lakini watakaonufaika ni wanaume kwa sababu ndiyo wanaomiliki ardhi kwa asilimia kubwa tofauti na wanawake," alisema.

# Iringa walivyojipanga kutokomeza ukatili kijinsia

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

WADAU mkoani hapo wameanza kuchakata jumbe mbalimbali zitazobandikwa katika maeneo ya kutolea huduma ili kusaidia kupunguza vitendo vya ukatili wa kijinsia (GBV).

Akizungumza na Napishe jana, Meneja wa mradi wa watoto wenye watoto (CwC), unaotekelezwa na Shirika la SOS Children's Villages Tanzania (SOS CV), Victor Mwaipungu, alisema mchakato wa kutengeneza jumbe hizo unahusisha idara mbalimbali ikiwamo elimu, maendeleo ya jamii, ustawi wa jamii, viongozi wa dini, jamii pamoja na vyombo vya habari.

Alisema zitasaidia kupeleka ujumbe kwa upana katika jamii kupinga vitendo vya ukatili wa wanawake na watoto.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mkoa wa Iringa, Martin Chuwa, alisema walikuwa na kikao na wadau wanaotoa huduma za ustawi wa jamii mkoani humo ambacho kilikuwa na lengo la kutengeneza jumbe ambazo zitachagiza kuzuia vitendo vya ukatili wa kijinsia na vitendo vya ukatili dhidi ya watoto (VAC).

Alisema kuwa jumbe hizo zimelenga makundi yote katika jamii, kama waendesha bodaboda na bajaji, wananchi, wazazi na walezi, walimu, mashehe na wachungaji.

Kuhusu hali ya ukatili katika Mkoa wa Iringa, Chuwa alisema vitendo vya ukatili vinaongezeka kwa vile matukio mengi yalikuwa hayaripotiwi na baada ya elimu ya muda mrefu yanaonekana kuripotiwa kwa wengi.

Alifafanua kuwa takwimu zilizoko kila baada ya miezi mitatu matukio yanafikia 542 hadi 556.

Alisema, kati ya hayo asilimia 47 ni matukio ya ukatili dhidi ya watoto.

Chuwa aliongeza kuwa kitaifa, Mkoa wa Iringa unaongoza kwa kuhukumu kesi za ukatili mahakamani kila wiki wanapata hukumu tatu hadi nne.

Diana Lawa (20), mmoja wa wanufaika wa mradi wa CwC, kutoka Wangama katika Kata ya Luhota, wilayani Iringa alisema kuwa mradi huo umewasaidia kutoka hatua moja hadi nyingine.

Alisema kabla ya mradi walikuwa mitaani bila kuwa na kitu cha kufanya, lakini baada ya SOS CV kuwainua kwa sasa kuna uhafadhali kwa kuwa wameweza kujitambua.

Alisema baada ya mradi huo wamefanikiwa kuunda vikundi vya ujasiriamali ambavyo vinasajiliwa na kuunganishwa na fursa mbalimbali zinazotolewa na halmashauri kupitia mikopo ya asilimia kumi.

Mikopo ya halmashauri inatolewa kwa makundi mbalimbali kama vile vijana, wanawake, wazee na wenye ulemavu kutokana na asilimia 10 ya mapato yake ya ndani (own source).

Pia ukosefu wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana ni chanzo kikubwa cha vijana wa kike kupata mimba katika umri mdogo na hatimaye kukatisha masomo.

"Mimi mwenyewe nina watoto wawili ambao nilizaa katika umri mdogo kutokana na kukosa elimu ya afya ya uzazi wakati huo. Mtoto wa kwanza nilimzaa wakati nipo kidato cha kwanza, wa pili nilimpata kwa bahati mbaya..." alisema.


Ukurasa 13

WAHADZABE -2

## Wahadza ‘wanasayansi asilia’ wanaojua kila hazina msituni


Nipashe

# TESA

Jumanne Septemba 13, 2022

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 12

## Ukosefu teknolojia unavyoifanya Afrika kuwa jumba la maradhi

ELIMU


NA PANKRASI LUOGA


# Ndivyo wazazi, walezi kuwasakia watoto ajira kunavyozalisha jeshi la wasiowajibika


Kinamama na watoto mgongoni wanasimama bila huduma kwa muda mrefu. Moja ya sababu huenda ni uzembe, kutokujali wala kuwajibika kazini pengine kunakotokana na kijana kutumikia kazi asiyoipenda. **PICHA: MTANDAO**

MZAZI au mlezi anapokwenda kumtafutia ajira mtoto wake, ile kazi anaifanya nani ni yeye au mtoto? Na hivyo nani atakuwa na uchungu nayo zaidi kati ya hao? Tukiwa bado tunatafakari swali hilo ni wazi kuna madhara katika hilo.

Ndiyo maana utawaona wengi maofisini, hawajali kazi, wanachati muda wote, wanaongea na simu janja, kila wakati, wanapotoka ofisini hawarudi lakini wanapenda zaidi pesa bila kujali kuwa hawajafanyakazi.

Tuangalie suala la wazazi au walezi kuwatafutia watoto ajira, kwa sasa shule na vyuo nchini vinazalisha wahitimu wengi tena wenye ujuzi wa aina mbalimbali. Hata hivyo, wengi hawapati kazi kwa wakati kadiri ya matarajio hasa yale yanayotokana na hadithi za darasani kuwa mafanikio ya watu waliosoma kozi au fani hii au ile yanakuja haraka. Tatizo hilo huwakumba vijana wengi walijiwekea malengo ya kimaisha ambayo hutegemea kuyatimiza kwa kuajiriwa na kupata mishahara.

Kukosa ajira kunawalazimisha wazazi na walezi kuguswa na ukosefu wa kazi kwa watoto wao na kujitwika jukumu la kwenda huku na kule kuwasaidia, wapo ambao huenda kwa watu wao wa karibu na wanaowafahamu na kuongea nao na hivyo watoto wao kupata ajira kiurahisi bila jasho.

Lakini, kwa upande mwingine mambo huwa magumu hasa kwa wazazi na walezi ambao hawana rafiki wenye shughuli au miradi inayoweza kuwaajiri watoto wao. Hubaki wakiumia na kukosa sehemu ya kuwapeleka, hivyo watoto hao hubaki nyumbani wakiwa hawana kazi au kupata ajira kwa juhudi zao wenyewe.

Wale ambao wazazi au walezi wao huwatafutia ajira na kuajiriwa kwa njia ya kujuana au wazazi kuwaombea ajira wakati huo wao hawajishughulishi wala kuhangaika na kutafuta kazi, ni nini hatima yao.

### HASARA KWA MTOTO

Kuna faida na hasara za kutafutiwa kazi na wazazi, walezi au jamaa, kuna faida moja mbayo ni kupata kazi bila kutoa jasho wala juhudi zozote ziwe kwa maneno au kutembea na vyeti. Kupata ajira kwa urahisi au kiulaini.

Kwa upande wa hasara ziko nyingi kabla ya kuzitaja ni vyema kujiuliza; mzazi au mlezi anapotafuta kazi ya mtoto ataifanya nani? Na kama ni mtoto na sio aliyeitafuta baadhi ya matokeo mabaya ni pamoja na aliyeombewa kazi kuifanya bila juhudi kwani aliyeipata kirahisi bila juhudi hivyo hana uchungu wowote, au hakuipenda na hivyo kukosa mapenzi nayo.

Kutojali wala kuheshimu kazi na kuwa na imani kuwa ana mtetezi maana mzazi au mlezi yupo kuendelea kubembelezea. Lugha chafu kwa wateja hazitaisha wala uzalishaji wa bidhaa au huduma hauwezi kupanda kwa maana wafanyakazi wanaotarajiwa kuzalisha au kutoa huduma hawapendi kazi yao hiyo.

Kadhalika watu wana ushuhuda wa vituko maeneo ya kutolea huduma ikiwa na pamoja na lugha za matusi, kuongea au kuchati na simu muda mrefu au kutoa lugha za kejeli na wafanyakazi kujali zaidi mambo yao binafsi kuliko ya wananchi kwani wao ndio wateja wanaonunua bidhaa au huduma na wao kulipwa mishahara yao.

Mfano, saa 2:00 au 3:00 asubuhi mtumishi wa umma baada ya kufika kazini anasema kwanza ngoja nikanywe chai nikirudi nitakuhudumia halafu akitoka hapo kwenda kwenye chai basi kurudi ni baada ya kupita saa moja au zaidi. Na kuwaacha wateja wake wenye kuhitaji huduma hiyo wakisubiri toka asubuhi mpaka jioni na pengine huambiwa waje kesho tena.

Tukumbuke huu ni ukosefu mkubwa wa kujali na ukarimu kwa wale wanaowahudumia. Je, kweli unaweza kuchati na simu mbele ya bosi wako huku akisubiri umhudumie?

Hili limekuwa somo gumu kwa wafanyakazi wengi hasa wafanyakazi wa umma maana bado hawajatambua umuhimu wa wale wanaowahudumia. Baadhi yao ni kwasababu walitafutiwa ajira hizo na ndugu zao na hivyo kufanya kazi bila kuwa na mapenzi ya dhati katika kile wanachokifanya.

Na zaidi wengine hutumia ajira zao hizo kuwaibia wananchi ambao ndiyo mabosi wao kwa maana mishahara wanayolipwa inatokana na kodi za wananchi


INAENDELEA UK.14

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

# Ukosefu teknolojia unavyoifanya Afrika kuwa jumba la maradhi

TANGU mgonjwa wa kwanza wa maradhi ya vidonda vya homa ya ndui ya nyani (MPX) aripotiwe mwaka 1970, kumekuwa na milipuko kadhaa ya ugonjwa huo unaotikisa Afrika ya Kati na Magharibi na kuonekana kuwa hilo ni tatizo lao.

Kama yalivyo magonjwa mengine ya virusi, kipimo kwenye sampuli hugundua DNA ya virusi na kuanza matibabu, lakini wasiwasi ni kwamba mlipuko wa mwaka huu umeathiri maeneo mengi duniani. Ingawa vipimo vya uthibitisho wa MPX vinapatikana duniani kote, uwezo wa Afrika kutambua na kudhibiti ugonjwa huo ni changamoto kubwa hasa sasa.

Changamoto zinazokabili Afrika ni pamoja na ukosefu wa miundombinu ya kutosha ya maabara na wafanyakazi wa afya wanaofahamu MPX, mifumo dhaifu ya ufuatiliaji wa magonjwa na ukosefu wa ufahamu wa MPX miongoni mwa wafanyakazi wa afya na jamii.

Hadi mwaka huu, ndui ya nyani au 'monkey pox' iliripotiwa kuzuka na kuua watu Afrika na haijawahi kuripotiwa nje ya bara hilo. Hata hivyo ilizuka Ulaya na Amerika na kusababisha dunia nzima kuamka na kushughulia tatizo hilo na Afrika kupata mkombozi. Tiba ya ugonjwa huo ni changamoto Afrika kwa sababu hakuna utaalamu, utafiti na zaidi fedha za kukabiliana na maradhi hayo.

Ni ugonjwa unaoripotiwa Afrika ya Kati na Magharibi, mara nyingi karibu na misitu minene yenye mvua muda wote ya kitropiki. Lakini mara kwa mara ndui ya nyani imetinga hadi mijini. Inawakamata wanyama kama panya na nyani.

Chanjo ya ugonjwa huo unaosambaa kwa virusi iliyopitishwa mwaka 2019, iko kwenye mataifa yaliyoendelea, lakini upatikanaji wake bado ni changamoto kubwa hasa Afrika ambako teknolojia na utafiti ni eneo linalokabiliwa na vikwazo vingi.

Awali chanjo zilizotumiwa wakati wa mpango wa kutokomeza ndui pia zilitoa kinga dhidi ya 'monkey pox.' Chanjo mpya zaidi zilitengenezwa na moja kuidhinishwa kwa ajili ya kuzuia magonjwa hayo, hata hivyo Shirika la Afya Duniani WHO- linasema, upatikanaji wake bado ni mgumu mno.

Ndui ya nyani husababishwa na virusi vya 'monkeypox' na kwa kawaida dalili hudumu kwa wiki mbili hadi nne na katika siku za hivi karibuni, uwiano wa vifo umekuwa wastani wa asilimia tatu mpaka sita.

Maambukizi ya ugonjwa huo kwa binadamu yanatokea kukiwa na ukaribu na wanayama hao, lakini pia virusi huambukizwa kutoka kwa mtu hadi mwingine kwa kugusana kwa karibu na vidonda, maji maji ya mwili, makamasi, kulalia vifaa vyenye maambuki kama vile matandiko na mashuka. Tofauti na COVID-19 iliyoanzia China na kuendelea Ulaya na Amerika na baadaye kuripotiwa Afrika, ndui ya nyani au vidonda ya 'monkeypox' ni maradhi yaliyoua Waafrika wengi.

WHO iliitangaza homa hiyo ya monkeypox kuwa ni kitishi cha afya ya umma duniani na kwamba mataifa yanapaswa kushirikiana kukomesha haraka kuenea kwa ugonjwa wa ndui ya nyani. WHO inahimiza juhudi zifanyike kutokomeza maradhi hayo bila kujali utaifa, rangi ya mtu au dini.

Ni kauli ya Dk. Ibrahima Soce Fall, Mkurugenzi Msaidizi wa WHO, anayehusika na masuala ya dharura anasema hayo wakati akizungumza na wanahabari huko Geneva, Uswisi, kuelezea kuhusu jinsi vifo nje ya Afrika, vilivyoiamsha dunia kushughulikia ugonjwa huo.

Kama ilivyokuwa kwa ugonjwa wa zika, kuibuka kwa ugonjwa huu nchi za Ulaya ndiko kumesababisha dunia nzima sasa kuwa makini kuhusu homa ya ndui ya nyani. Dk. Soce Fall, anaeleza kuwa kuingia ndui ya nyani Ulaya kumeamsha watu wengi na kukumbusha kuwa WHO imekuwa ikishughulikia ndui ya nyani barani Afrika kwa miaka kadhaa lakini hakuna mtu yeyote ambaye alitilia maanani.

"Ugonjwa huu kwa bahati mbaya uliwekwa kwenye kundi la magonjwa ya kitropiki yanayopuuzwa, tulihangaika na rasilimali chache na ilihitajika nchi zilizoendelea nazo ziambukizwe ugonjwa huu ili dunia ichukue hatua. Ndivyo ilivyokuwa kwa zika na lazima tukomeshe ubaguzi huu wa kushughulikia matibabu na majanga duniani," anasisitiza Dk. Fall.

Julai 23, mwaka huu WHO ilitangaza kuwa ndui ya nyani ni ugonjwa unaohitaji kuangalia kama tatizo la dharura la afya ya umma duniani, hatua ambayo inalenga kuwezesha shirika hilo kuratibu na kushirikiana na nchi na wadau halikadhalika mshikamano wa kidunia kuukabili ugonjwa huo.

Lakini kwa upande mwingine WHO inaeleza kuwa maambukizi barani Ulaya na Amerika Kaskazini, yamo miongoni mwa wanaume mashoga wenye wapenzi wengi.

"Dunia lazima ichukue hatua kulinda jamii bila kujali utaifa, rangi yao au dini zao. Nadhani ni muhimu sana tena sasa ambapo zaidi ya nchi 70 zina ugonjwa huo hivyo kila mtu anajishughulisha." Shirika hilo limetangaza kuwa mlipuko wa ndui ya nyani au monkeypox duniani ni tishio kwa afya ya umma.

Mkurugenzi Mkuu wa WHO Dk. Tedros Ghebreyesus, ndiye anayesema akizungumza kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa ndui ya nyani. Takribani nchi 45 ziliripoti kushambuliwa na maradhi hayo na kwamba tathmini ya WHO anaonyesha kuwa hatari ya ndui ya nyani ni ya kati (siyo ya kutisha sana) na katika kanda zote isipokuwa kanda ya Ulaya ambako hatari ni kubwa zaidi. Halikadhalika kuna hatari dhahiri ya kusambaa zaidi kimataifa, ijapokuwa hatari ya kuvuruga safari za kimataifa bado kwa sasa ni kidogo.

"Kwa misingi hiyo nimeamua kuwa mlipuko wa ndui ya nyani ni tishio la afya ya umma duniani. Nimeweka mapendekezo kwa makundi manne ya nchi. Ambazo hazijaripoti mgonjwa kabisa au ndani ya siku 21. Zile ambazo zimeripoti na zina maambukizi baina ya binadamu. Hawa wachukue hatua kudhibiti mlipuko." Anasema Mkurugenzi Mkuu wa WHO Dk. Tedros Ghebreyesus.

Kundi la tatu ni wale wenye maambukizi baina ya wanyama kwenda kwa binadamu na nne ni nchi zinazotengeneza vipimo vya uchunguzi, chanjo na matibabu.

*UN NEWS*


Mgonjwa wa vidonda vya homa ya ndui ya nyani. **PICHA: MTANDAO**

"Kundi la tatu ni wale wenye maambukizi baina ya wanyama kwenda kwa binadamu na nne ni nchi zinazotengeneza vipimo vya uchunguzi, chanjo na matibabu.

ELIMU

NA DR. FELICIAN KILAHAMA

WAHADZABE -2

# Wahadza 'wanasayansi asilia' wanaojua kila hazina msituni

SEHEMU ya kwanza ya makala hii ilieleza kuhusu maisha ya Wahadzabe wanavyoishi kwenye misitu iliyoko kwenye bonde la ufa sehemu ya Yaeda-Chini wilayani Mbulu mkoa wa Manyara.

Vilevile, ilifafanua walitoka wapi hadi kuishi hapo walipo na sababu zilizopelekea kufanya hivyo. Katika eneo la Yaeda Chini; misitu imesheheni aina mbalimbali za miti kwenye mfumo wa ikolojia aina ya 'Acacia-Commiphora'.

Makala hii inafafanua zaidi maisha ya Wahadzabe wanaotegemea rasilimali misitu kwa mwaka mzima ikiwa ni chanzo chao kikuu cha chakula na lishe.

Kimsingi Wahadzabe wanafahamu vizuri mazingira ya mahali wanapoishi pamoja na uelewa wa kina kuhusu wapi wanaweza kupata maji, asali, dawa na chakula. Aina na sehemu kilipo na lini kitapatikana, wanasema zaidi ya miaka 30 iliyopita, wanyama wakubwa mathalani tembo au nyati walikuwapo lakini sasa ni adimu kuwapata.

Ninapowauliza 'kwa nini wanasema hivyo' jibu lilikuwa 'ujangili umekuwa tishio sana kwa wanyamapori kama 'tembo'. Kawaida Wahadzabe hupata kitoweo kwa kuwawinda wanyamapori.

Vilevile, vyakula vyao vingine ni matunda, asali na viazi, mihogo pori. Wahadzabe niliozungumza nao wanasema kwa miezi ya Agosti na Septemba matunda hupatikana kwa wingi na wanao utaalamu wa kuyahifadhi kiasilia na kuyatumia kwa muda mrefu.

Vilevile, wanasema kuwa wanaithamini sana mibuyu kwa sababu ni chanzo muhimu sana cha lishe. Katika mibuyu wanapata matunda na unga baada ya kusaga matunda yaliyokauka vizuri. Kutokana na unga huo huweza kutayarishi uji. Kadhalika katika eneo la msitu wanapoishi huweza kupata viazi na mihogo asilia. Aina hiyo ya chakula huipata kutoka katika aina mbalimbali za miti na mimea inayostawi katika msitu.

Isitoshe, Wahadzabe wanasema kwamba 'asali ni zaidi ya vyakula maana ni kama benki ambako watu wengine hupata fedha kwa matumizi mbalimbali. Mathalani, watu wananunua chuma kutengeneza shoka, mishale, visu pia kununua nguo au viatu inapobidi kutokana na rasilimali zinazopatikana kwenye misitu.

Hata hivyo, asali zamani ilikuwa haiuzwi isipokuwa kuitumia kama chakula lishe kuimarisha miili yao. Ilibainika kuwa Wahadzabe wanauelewa mzuri wa wapi mahali pa kupata asali maana wao hawafugi nyuki bali wanatunza mazingira kuwawezesha nyuki kufanya kazi yao bila kubughudhiwa.



Dk. Felician Kilahama akifurahia mbuyu uliostawi ndani ya vichaka kutokana na kuhifadhiwa na Wahadza. **PICHA: MWANDISHI WETU**

Wanasema kwamba kulingana na misingi na utaratibu wa maisha yao, wanaume ndiyo wenye jukumu la kutafuta na kurina asali.

Isitoshe, wanaelewa wapi pa kupata asali kulingana na uhalisia wa msituni. Hata hivyo, wanawake wanaweza pia kurina asali pamoja na majukumu yao mengine kama kuchota maji, kutafuta na kuchimba viazi, mihogo asilia, kupika chakula na kuwatunza watoto.

Wanapoulizwa je, wapo nyuki wa kutosha katika eneo lao? Wanajibu 'ndiyo wapo' na baadhi ya aina ya nyuki waliopo wanawataja kwa mfano aina ya 'Awawa' ambao ni nyuki wa kawaida wanaouma, kitaalamu huitwa Apis Melliferaseulelata na kwa Kihadza ni Ba'alako.

Nyuki hawa hutengeneza asali nyingi na tamu. Aina nyingine ni 'kanowa' nyuki wasiouma au 'Trigonarus polsi' wanaeleza kuwa ni 'ba'ala ma kanowa' (nyukijasho) na kwamba asali yao ina ladha nzuri na tamu.

Aina nyingine ni 'Tsunako' and 'Nlateko' pia ni wasiouma wanawaita: ba'alasatsunako na trigonaglibodoi, na asali yao ni tamu. Kuna pia 'bambahau' au nyukijasho pia wasiouma lakini hukusanya asali kutoka kwa nyuki wengine na wadau wanasema asali yao ni tamu sana.

Aina ya mwisho waliyosema ni Lulindi (Ba'ala ma Lulindi) pia ni nyuki wasiouma ila rangi yao nyeusi na ukubwa wao kama inzi inasadikiwa kwamba wanatengeneza asali nyingi sana.

Pamoja na mahojiano na kutembezwa sehemu kadhaa msituni, taarifa zilizopo kuhusu Wahadzabe mfano, mwandishi Peterson na wenzake walioandika mwaka 2013, wanaonyesha kuwa Wahadzabe wanaelimu ya mazingira wanamoishi na wanaweza kutofautisha aina mbalimbali za asali na ubora wake kwa kuangalia hata bila kuonja.

Wanaufahamu vizuri mfumo wa ikolojia msituni, unavyosaidia kuotesha miti na mimea mbalimbali inayofaa kwa nyuki kutengeneza asali bora.

Mathalani, wanasema kuwa aina ya miti "mukanagako" au 'migunga' kwa Kiswahili na kitaalamu Acacia tortilis, hutoa maua kipindi cha Januari na Februari kuwezesha nyuki kutengeneza asali. Wanaongeza kuwa kwa wakati huo nyuki wanakuwa wakali zaidi ukilinganisha na miti aina ya "militimoko" au 'migunga' Acacia melifera, ambayo hutoa maua kwa kipindi kirefu zaidi.

> Wanaufahamu vizuri mfumo wa ikolojia msituni, unavyosaidia kuotesha miti na mimea mbalimbali inayofaa kwa nyuki kutengeneza asali bora.

Hivyo miti aina hii hufanya nyuki kuwa watulivu na rafiki hawasumbui binadamu hiyo ni kulingana na maelezo ya Wahadzabe.

Wanasema 'takribani miaka 60 iliyopita eneo la misitu Yaeda-Chini, limekuwa ni hazina kubwa ya chakula chao, kutokana na mifumo ya misitu ya Acacia-Commiphora; wamekuwa wakipata kitoweo cha wanyamapori, asali, matunda na mihogo au viazi asilia. Kadhalika, wanasema kwamba kwao mti muhimu sana ni 'mbuyu' kitalaamu huitwa Adansonia digitata wanautambua kama "nllobako".

Kulingana na maelezo yao, mibuyu inakuwa mikubwa na kutoa matunda mengi na juu kabisa hutengeneza nafasi ambazo nyuki wanaouma huzitunia kutengeneza asali.

Vilevile, wanasema kwamba wakila ubuyu, asali na nyama wanaamini kwamba miili yao inapata lishe kamili na inasadikiwa kwamba vitamini 'c' katika ubuyu ni mara sita zaidi ya chungwa; mara mbili zaidi ya 'calcium' inayopatikana kwenye maziwa.

Vilevile, ubuyu una 'potassium' ambayo ni muhimu kwa ubongo, mishipa ya fahamu 'neva' na misuli. Kuna pia 'phosphorus' inayohitajika kuimarisha mifupa na protini na mafuta kwa kujenga seli za mwili.

Kwa hali hiyo Wahadzabe wamekuwa ni wahifadhi mahiri wa maeneo au misitu wanamoishi.

Mathani, mzee moja anasema: "tunaamini kwamba misitu inao uwezo wa kututunza kwa kutupatia chakula, maji na dawa bila kuhangaika sana; ndiyo maana tumekuwa hatuna wasiwasi kuhusu kesho hususani tutakula nini maana tulikuwa na uhakika tutapata tunachokihitaji". Kinachomaanishwa hapa ni kwamba kwa Wahadzabe kila kukicha mambo ni mazuri isipokuwa eneo wanaloishi lenye ukubwa wa takribani hekta 40,000 litunzwe na kusimamiwa ipasavyo kwa faida ya jamii nzima ya Wahadzabe.

Wanasema mihogo au viazi pori vinapatikana kwa mwaka mzima na wanaweza kuvuna takribani tani 20 kwa mwaka. Baadhi ya mihogo na viazi pori hujulikana kama 'shumuko' Vilevile, miti wanapopata asali na ile inayofaa kuwasha moto wanaijua na inapatikana bila shida. Makala itakayofuata itaelezea zaidi kuhusu matunda, namna wanavyowasha moto, maisha yao kama jamii, na changamoto pamoja na nini kifanyike ili misitu iendelee kuwapo kama chanzo muhimu kwa Wahadzabe kuweza kuyamudu maisha yao ya kila siku.

# Ndivyo wazazi, walezi kuwasakia watoto ajira kunavyozalisha jeshi la wasiowajibika

INATOKA UK.11

hao ambao wale wanaotakiwa kuwahudumia na sio kujinufaisha wao na familia zao.

Tukumbuke wenye kukulipa mshahara wako ndiyo mwajiri wako anayekuwezesha kuishi na kuendesha maisha yako kwa kupata hela ya chakula, hela ya kulipa pango la nyumba, kupata hela ya ada, chakula na mengine.

Ni sawa na madhara ya mtoto kuchaguliwa na kulazimishwa kuolewa au kuoa mwenza asiyempenda ni sawa na kile kinachotokea kwa anayepatiwa ajira bila kujishughulisha wala kuwa na mapenzi ya dhati na kazi hiyo.

**UFUMBUZI WA CHANGAMOTO**

Wazazi na walezi wajitahidi kuwalea na kuwajengea watoto wao hali ya kujitegemea na kuwajibika kwa mambo yote yanayohusu maisha yao. Na hivyo wazazi wawaache watoto au vijana wao watafuate ajira wenyewe tena ajira zenye kazi wanazoweza kuzifanya na kuzipenda kwa kiasi kikubwa hivyo kutoa bidhaa au huduma zenye ubora unaotakiwa.

Wanaweza kuwashauri na kuwahimiza kubadilika zaidi waajiri nao waanze kujifunza kuwa watoto wanaotafutiwa



Wananchi wakisubiri huduma huku wakuwahudumia asiwepo. Kutojali watu ni baadhi ya matukio yanayosababishwa na vijana au wahusika kutokujali kazi hasa wale ambao walipewa ajira bila kuzisotea. **PICHA: MTANDAO**

kazi na wazazi wao sio watu wa kuwategemea katika kuongeza uzalishaji au ubora wa huduma katika taasisi zao. Kwani wao sio walitafuta na hawana uchungu na kazi hiyo.

Pia waajiri hao wanakosa muda wa kuwafanyia tathmini na ufuatiliaji japo ya haraka kwasababu wazazi na walezi ndiyo wanaokuja kuomba ajira. Mfano, akija mzazi kutafuta kazi ni tofauti sana na akifika kijana mwenyewe kwani wewe kama mwajiri unaweza hata kumwuliza maswali machache ili kupima uelewa wake, mtazamo wake kwenye kazi husika na pia mwonekano kama kweli ataweza kutimiza wajibu huo.

Katika kuwaachia jukumu hili la ajira kwa watoto ni muhimu walezi na wazazi wazingatie kwanza maandalizi ya msingi katika kuwatayarisha watoto wao kujitafutia ajira wenyewe kuwapa rasilimali wanazohitaji, kuwezesha utekelezaji wa hatua za kubadilisha rasilimali na kuwa bidhaa au huduma na kuchukua hatua za kurekebisha kasoro mapema ili kutoa mazao bora ambayo ni mafanikio ya kuwa na vijana wenye maadili mema, uelewa mkubwa na elimu nzuri tayari kwa kuweza kujitafutia ajira wenyewe katika jamii.

Wahakikishe watoto wanapata muda wa kupumzika, nafasi ya kujisomea na pia muda wa kucheza kwa kiasi, kunapata chakula, upendo, heshima, hii itasaidia watoto kujiandaa vizuri na kuwa na ujasiri wa kutosha kujitafutia kazi wenyewe bila kutegemea kutafutiwa.

Wito wangu kwa jamii ni kuwa wazazi na walezi wawaandae watoto wao kikamilifu kwa kuwapa elimu, upendo, heshima na vyote venye kuhitajika ili kumwezesha kuwa na ujasiri wa kutafuta ajira yake mwenyewe na kufanya kazi kwa juhudi na maarifa bila kutegemea msaada wa wazazi au walezi.

Wanaohusika na mambo ya kuajiri wafanyakazi wawe makini na wazazi wanaotafuta kazi kwa niaba ya watoto wao na kwani watoto hao hawana elimu, maarifa na mapenzi na kazi hiyo hivyo kushindwa kuifanya kwa ufanisi unaotakiwa.

Na mwisho hii itasaidia waajiriwa wengi vijana wasisahau kuwa wananchi wanao wahudumia ndio waajiri wao hivyo ni lazima kuwahudumia kwa moyo wote, juhudi hizo zitaongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa na huduma zitolewazo nchini hasa kutoka serikalini na taasisi umma.

*Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi wa Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Afya - MUHAS*

## WANENAVYO MALENGA

### VITU LAINI LAINI

Watu wengi siku hizi, hukwepa vitu vigumu,
Wanakacha zile kazi, wazionazo ni ngumu,
Wanakwepa utatuzi, hata yaliyo muhimu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Hata kama ni chakula, hukwepa kile kigumu,
Ugali kwa shida wala, ila chipsi ni tamu,
Ule unalimwa Kyela, wabugia bila zamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Kazi ya shamba kulima, kwa uchumi ni adhimu,
Kila mtu anasoma, kwingine akajikimu,
Kubeti wanajituma, kwa sababu pesa tamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Watu wanasema sana, tadhani ni watalamu,
Sasa na wao kutana, ikibidi kama timu,
Pamoja mkiungana, kuandika kwa kalamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Kuku mifupa mifupa, zama zile nyama tamu,
Unashika lako fupa, tafuna iishe hamu,
Sasa sawa na kukopa, minofu ndiyo mitamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Changamoto zaibuka, ni kulaumulaumu,
Badala kuwajibika, kwenda mbali wajihimu,
Baadaye wakifika, wazidi kucheza gemu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Watu wanapewa miwa, juisi yake ni tamu,
Ila kutafuna miwa, meno yao ni vigumu,
Visu ndiyo hutumiwa, acha meno yale sumu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Ule wimbo dezo dezo, muda wake umetimu,
Watu wenye uwezo, waja watu kukaimu,
Umri kwao uozo, hao wengi wamo humu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Wanachopenda kulishwa, hata matunda damu,
Ikibidi kuvalishwa, waume kama mademu,
Ni kama wameloweshwa, na kukosa ufahamu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

Ili uwe ni mshindi, upambane na magumu,
Huja vipindivipindi, sawasawa na swaumu,
Na wewe jaza ufundi, mwishowe utahitimu,
Vitu laini laini, watu wanakimbilia.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### LAKINI HII BARIDI

BaridI ina upepo, si ya kustahimili,
Inanifwata nilipo, nina blanketi mbili,
Kunyosha mkono, kwangu inakuwa ghali,
Dirisha naacha wazi, miye nawasha mkaa.

Dirisha naacha wazi, miye nawasha mkaa,
Ni tahadhari hizi, ile ya hewa ukaa,
Isifanye fumanizi, na uhai ukapaa,
Baridi ya mwaka huu, kama yavunja rekodi.

Baridi ya mwaka huu, kama yavunja rekodi,
Hasa kwa nyanda za juu, ni kama wameikodi,
Joto kama wanukuu, barafu huku zawadi,
Kama ni tabia nchi, inabadilika sana.

Kama ni tabia nchi, inabadilika sana,
Onyo kwetu wananchi, tuipande miti sana,
Zile mbao za makochi, miti zinachanachana,
Tukitunza mazingira, hali itakuwa nzuri.

Tukitunza mazingira, hali itakuwa nzuri,
Hatutapata hasara, hali ya hewa hatari,
Tutapanga zetu sera, hata kuishi vizuri,
Hata kule Dasalamu, baridi yake ni mpya.

Hata kule Dasalamu, baridi yake ni mpya,
Mashuka sasa matamu, na mablanketi mapya,
Kuvaa koti muhimu, utanashati na afya,
Hali imebadilika, na sisi tubadilike.

Hali imebadilika, na sisi tubadilike,
Yale yalizoeleka, mazingira yachafuke,
Ni bora yakafutika, na sisi tusiteseke,
Kuyatunza mazingira, ni kujipenda wenyewe.

Kuyatunza mazingira, ni kujipenda wenyewe,
Kuharibu ni hasara, nayo ya kwetu wenyewe,
La kufanya la busara, chaguo letu wenyewe.
Lakini hii baridi, kuna mkono wa mtu.

Lakini hii baridi, kuna mkono wa mtu,
Nyumbani ile akidi, inakidhi roho kwatu,
Kuchelewa makusudi, kumekwenda na msitu,
Viti virefu vifupi, baridi havina watu.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





## NBS yataja kiini mfumuko wa bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), imesema mfumuko wa bei wa taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2022, umeongezeka hadi asilimia 4.6 kutoka 4.5 kwa mwezi Julai 2022.

Ongezeko la mfumuko huo limechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula ikiwamo unga wa mahindi kutoka asilimia 19.3 hadi 37.2.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mtakwimu Mkuu wa Serikali jana, ongezeko hilo linamaanisha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwezi Agosti imeongezeka kulinganishwa na kasi ya mwezi Julai mwaka huu.

Bidhaa zingine za vyakula zilizoonyesha kuongezeka kwa mfumuko huo ni ngano kutoka asilimia 3.7 hadi sita, nyama kutoka asilimia -4.3 hadi 5.1, mboga kutoka asilimia moja hadi 2.7.

Maharage kutoka asilimia 1.9 hadi 2.7, mihogo mikavu asilimia nane hadi 8.4 na unga wa muhogo kutoka asilimia 9.5 hadi 10.9.

Taarifa hiyo pia imebainisha mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2022, umeongezeka hadi asilimia 7.8 kutoka asilimia 6.5 kwa mwaka ulioishia mwezi Julai 2022.

Hata hivyo, mfumuko wa bei ambao haujumuishi bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Agosti 2022, umepungua kidogo hadi asilimia 3.4 kutoka asilimia 3.8 ilivyokuwa mwezi Julai 2022.

Kwa nchi za Afrika Mashariki, Uganda mfumuko kwa kipindi hicho umeongezeka hadi kufikia asilimia tisa kutoka asilimia 7.9 kwa mwaka mwezi Julai 2022.

Mfumuko wa bei Kenya kwa mwaka ulioishia mwezi Agosti 2022, umeongezeka hadi asilimia 8.5 kutoka asilimia 8.3 kwa mwaka ulioishia Julai 2022.

**Maharage kutoka asilimia 1.9 hadi 2.7, mihogo mikavu asilimia nane hadi 8.4 na unga wa muhogo kutoka asilimia 9.5 hadi 10.9.**

# Waziri aagiza utekelezaji kutokutoza ushuru mazao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa ameziagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zinatekeleza mwongozo wa serikali wa kutotoza ushuru kwa wakulima wanaosafirisha mazao yao chini ya tani moja.

Bashungwa aliagiza hayo mwishoni mwa wiki jijini hapo alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mwongozo wa kutotoza ushuru kwa wakulima wanaosafirisha mazao chini ya tani moja.

Alisema katika kuweka mazingira rafiki na wezeshi kwa wakulima, serikali ilitoa maelekezo ya kuhakikisha wakulima hawatozwi tozo wanaposafirisha mazao yao kutoka shambani kwenda kwenye magulio.

"Mpaka sasa bado maagizo ya serikali ya kutotoza ushuru wakulima wanaposafirisha mazao yao chini ya tani moja hayajabadilika.

"Maelekezo ya serikali ni kuhakikisha wakulima wanapovuna na kupeleka mavuno ya mazao kwenye magulio na masoko kama ni chini ya tani moja, wasitozwe ushuru wowote," alikumbusha.

Bashungwa alimwagiza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe kuhakikisha mwongozo huo unazingatiwa na wakurugenzi wote nchini.

Waziri huyo pia alielekeza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kusimamia mwongozo huo katika maeneo yao.

"Nitumie nafasi hii kuwaelekeza wakuu wa mikoa na wa wilaya katika maeneo yao kusimamia jambo hili ili lisifanyike kiholela kwa maeneo mengine wanatoza na maeneo mengine hawatozwi. Kwa hiyo, kunakuwa na mkanganyiko upande wa wakulima lipi ni lipi.

"Katika kutekeleza agizo hilo la serikali, Ofisi ya Rais -TAMISEMI ilitoa mwongozo kwenye halmashauri zote namna ya kulitekeleza, hivyo niwakumbushe wakurugenzi kuendelea kuzingatia mwongozo huo na wakuu wa mikoa na wilaya simamieni jambo hili, lengo ni kumsaidia mkulima akue na kupambana na umaskini kupitia jasho lake la kilimo," aliagiza.

Waziri Bashungwa alisema serikali iliona ni vyema kuhakikisha ushuru kwa mkulima wa mazao chini ya tani moja hautozwi na inaendelea kuyasimamia kupitia wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kuhakikisha mwongozo huo unazingatiwa.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi (katikati), akipokea nyaraka kwa Manuela Dieng (kushoto), kutoka Taasisi ya Kimataifa ya African Legal Support Facility (ALSF) ya nchini Ivory Coast jijini Dodoma jana, walipofika kwa ajili ya mazungumzo. Kulia ni Aida Sylla kutoka taasisi hiyo. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Daktari: Wanaojaribu kujiua wasishtakiwe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MADAKTARI wanaotibu magonjwa ya afya ya akili, wameiomba serikali kupitia upya sheria inayowafunga watu wanaofanya jaribio la kujiua ili wapatiwe tiba na kuondoa tatizo hilo kwa jamii.

Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Huduma ya Ubora wa Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Akili Mirembe, Dk. Minael Urio, alitoa rai hiyo juzi baada ya hitimisho la matembezi ya hisani ya kupinga kujiua.

Alisema, waathirika hao wanapaswa kupelekwa hospitalini kupata matibabu ili kubaini tatizo linalowasumbua mpaka kufikia hatua ya kutaka kujiua.

"Wakipata nafasi ya kutibiwa, inaweza kusaidia kumtoa katika hatua aliyofikia badala ya kubaki vivyo hivyo akiwa mahabusu. Tunaomba sheria iangaliwe upya ili kuwanusuru waathirika wa matukio haya nchini," alishauri.

Dk. Urio, alisema wataalamu hao wanaamini wagonjwa wa afya ya akili wakipatiwa matibabu, watapona na kuendelea na majukumu yao vizuri.

"Ulimwenguni takriban watu 800,000 hujiua kila mwaka kutokana na sababu mbalimbali na kila baada ya sekunde 40 watu hufanya jaribio la kujiua," alisema.

Pamoja na hayo, aliishukuru serikali kwa kuwapatia bajeti kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya hospitali hiyo ambayo ni kitovu cha masuala ya magonjwa ya akili nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala, alisema matembezi hayo ni moja ya kigezo cha kuamsha hamasa kwa jamii ili kuwafichua wagonjwa wa akili na kuwapeleka kupata matibabu.

"Matembezi ya hisani yamesaidia kwa kiasi kikubwa sana hospitalini hapa, tumefanikiwa kupata mabalozi ambao husaidia kutoa elimu ya kuwapeleka wagonjwa wa afya ya akili kupata matibabu," alisema Dk. Lawala.

Mbunge wa Iringa, Jesca Msambatavangu, aliipongeza hospitali hiyo kwa jitihada inazofanya kuhakikisha wagonjwa wa afya ya akili wanapatiwa matibabu.

Alisema, wabunge watalisemea bungeni suala la uboreshaji miundombinu ya hospitali hiyo ili kuhakikisha linatekelezwa ipasavyo kwa kuwa sehemu hiyo ni muhimu kwa jamii.

Pia, alisema watakwenda kutoa elimu kwa jamii katika maeneo mbalimbali katika majimbo wanayotoka ili jamii iwapeleke hospitali wagonjwa hao.





# Dk. Mpango aipa siku 10 TANROADS ujenzi mradi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa siku 10 kwa Wakala wa Barabara (TANROADS) kukamilisha ujenzi wa kituo cha ukaguzi wa magari katika eneo la Inyala, nje kidogo ya Jiji la Mbeya.

Alitoa agizo hilo juzi, alipotembelea eneo hilo ambalo ajali nyingi zimekuwa zikitokea mara kwa mara na hivi karibuni zilitokea na kugharimu maisha ya watu ikiwamo ya lori lililoyagonga magari mengine matatu na kusababisha vifo vya watu 19 na kujeruhi wengine 29.

Dk. Mpango, alisema endapo maofisa wa wakala huo hawatakamilisha kituo hicho ndani ya siku alizowapa, watakuwa wanamtafuta mambo mengine, akisisitiza ajali ambazo zimekuwa zikitokea, zimekuwa zikimkera.

Alisema, inamkera yeye binafsi kupokea na kumpelekea Rais taarifa za vifo vya watu vinavyosababishwa na ajali, akikumbusha kuwa baada ya kutokea ajali ya awali iliyoua watu 19, ilitokea nyingine iliyoua watu sita na kujeruhi wengine kadhaa.

"Hizi ajali zinatuhuzunisha sana kwa sababu zinagharimu maisha ya Watanzania wenzetu. Kwa hiyo, hakikisheni mnakamilisha kituo hiki ili malori kabla ya kuanza kuteremka hapa yakaguliwe kwanza mifumo ya breki," aliagiza.

Dk. Mpango pia aliutaka wakala huo ukamilishe ujenzi wa barabara ya mchepuko yenye urefu wa kilomita mbili katika eneo hilo ili kupunguza msongamano wa magari kwenye mteremko huo.

Alisema mbali na kuwaagiza maofisa hao, pia atampa maelekezo maalum Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ili kuongeza kasi ya ujenzi wa miradi hiyo.

Katika hatua nyingine, Dk. Mpango amemwagiza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kupeleka Sh. milioni 100 katika Zahanati ya Kijiji cha Shamwengo ambayo inajengwa kwa nguvu za wananchi kwa ajili ya kukamilisha mradi huo. Alitoa maelekezo hayo baada ya wananchi wa eneo hilo kuzungumza naye na kubainisha kuwa zahanati hiyo ingeweza kuokoa maisha ya baadhi ya watu wanaopata ajali kwenye mteremko wa Inyala kutokana na kuwa jirani nao.

Alisema, fedha hizo zitafutwe ndani ya wiki moja zipelekwe na ujenzi wa zahanati hiyo ukamilike mapema ili huduma zianze kutolewa haraka huku akiwapongeza wananchi kwa kujitolea kufanikisha mradi huo.

Akielezea hatua zilizochukuliwa na uongozi wa mkoa kukabiliana na ajali ambazo zimekuwa zikitokea kwenye mteremko huo wa Inyala, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera, alisema walikubaliana magari makubwa na madogo yapite kwa awamu.

Alisema, walikubaliana kutumia utaratibu huo kwa sababu umezaa matunda kwenye maeneo mengine ikiwamo kwenye Mteremko wa Mlima Iwambi ambapo pia ajali nyingi zilikuwa zinatokea miaka ya nyuma.

"Lakini kwenye hili eneo tuna mpango wa kutengeneza eneo lenye mwinuko ambapo malori yanayofeli breki yatakuwa yanapanda ili kupunguza mwendo, tulishaongea na wenzetu TANROADS wanalifanya hilo," alisema Homera.

Mmoja wa wananchi wa Kijiji cha Shamwengo, Joseph Kyombo, alisema baadhi ya watu wanaopata ajali katika eneo hio, huwa wanapoteza maisha kutokana na kukosa huduma ya kwanza mapema kutokana na vituo vya kutolea huduma kuwa mbali.

Alisema, kwenye ajali ya mwisho ambayo iliua watu sita, kuna mmoja angeweza kupona kama angepatiwa huduma ya kwanza mapema na hivyo akaomba serikali iwasaidie kukamilisha zahanati ya kijiji isaidie kutoa huduma kwa watu wanaopata ajali.

## Aita wadau ujenzi ofisi ya CHADEMA

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

ALIYEKUWA Diwani wa Ndato katika Halmashauri ya Rungwe, mkoani Mbeya, kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Paulos Zambi, amewaomba wadau wa maendeleo kuchangia ujenzi wa ofisi ya chama hicho unaoendelea katika kata hiyo ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Alitoa rai hiyo wakati wa harambee ya kuchangia ujenzi huo, akibainisha wanahitaji Sh. milioni 17, kwa ajili ya kukamilisha mradi huo.

Zambi, alisema wamekuwa wakichangishana kwa nyakati tofauti na mradi huo ulikwama miaka miwili iliyopita baada ya mhamasishaji wake (yeye mwenyewe) kuwekwa rumande kwa sababu ambazo hakuziweka wazi.

"Wananchi wa eneo hili wamekuwa wakiuza mazao yao na mifugo kwa ajili ya kuchangia mradi huu. Kwa hiyo, hapa tulipofikia tunahitaji nguvu za ziada ili tukamilishe, tunawaomba wadau mbalimbali watuunge mkono," alisema.

John Mwambigija, aliyewania ubunge wa Rungwe, kupitia CHADEMA katika Uchaguzi Mkuu uliopita, alisema ofisi za chama ni muhimu kujengwa kwa kuwa zinasaidia kusogeza huduma kwa wananchi.

Alisema, Kata ya Ndato imeonyesha mfano mzuri kwenye ujenzi wa ofisi za chama kwa kuwa ni miongoni mwa kata ambazo wanachama wa chama hicho wanajitolea kwenye shughuli za chama.

Alisema, kwa sasa katika Jimbo la Rungwe, kuna kata nyingi lakini ambazo zinaongozwa na madiwani wa chama hicho ni mbili tu ambazo ni Kiwira na Swaya.




Meya wa Jiji la Mbeya, Dormohamed Issa (kulia), akikabidhi mfano wa ufunguo kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Murshid Ngeze (kushoto) na Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Elirehema Kaaya, kuashiria ukaribisho wa viongozi hao jijini humo, ambako mkutano mkuu wa 36 wa jumuiya hiyo unafanyika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ghala lilivyookoa wakulima wa vitunguu

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

WAKULIMA wa vitunguu katika Skimu ya Umwagiliaji ya Igomelo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamepunguza upotevu wa mazao yao kwa zaidi ya asilimia 85 baada ya kujengewa ghala la kisasa.

Wakulima hao walikuwa wanapoteza mazao yao kutokana na kuoza baada ya mavuno kulikochangiwa na kutokauka vizuri, hasa kipindi cha masika.

Ghala hilo limejengwa na Shirika la HELVETAS, kupitia mradi wa KIBOWAVI ambao ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa Mnyororo wa Thamani wa Kahawa, Chai na Mazao ya Bustani, ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT.

Wakulima hao walibainisha mafanikio hayo juzi wakati wa ziara ya maofisa wa HELVETAS kwa ajili ya kukagua maendeleo ya Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Skimu hiyo cha Igomelo AMCOS.

Mwenyekiti wa Skimu ya Igomelo, Nelson Peter, alisema kabla ya kujengewa ghala hilo, wakulima walikuwa wanapoteza mazao yao ambayo yalikuwa yanaoza yakiwa kwenye maghala yao ya kienyeji.

Alisema, mbali na kuoza mazao mengine pia yalikuwa yanapotea kwa kuanguka chini, hivyo kuwatia hasara kubwa kutokana na gharama za uzalishaji kuwa kubwa.

"Tunawashukuru wenzetu Shirika la HELVETAS, kwa kutusaidia ghala hili maana kwa uwezo wa chama chetu tusingeweza kujenga na tungeendelea kupoteza mazao yetu kila wakati," alisema Peter.

Alisema, mbali na kusaidiwa kujengewa ghala pia wamesaidiwa wataalamu wa kilimo ambao wanawapa mbinu za kuongeza uzalishaji wa vitunguu kwenye skimu yao.

Baadhi ya wakulima hao walisema ghala hilo limewasaidia kuwa na eneo la uhakika la kuhifadhi mazao yao wakati wakisubiri soko liwe zuri, hasa katika kipindi ambacho soko linakuwa halijatengamaa.

Mmoja wa wakulima hao, Julius Kumwenda, alisema kabla ya kujengewa ghala hilo, walikuwa wanalazimika kuuza mazao yao kwa bei ya chini kwa hofu ya mazao yao kuoza.

Alisema, maghala waliyokuwa wanayatumia yalikuwa ya kienyeji kiasi kwamba wengine walikuwa wanapoteza zaidi ya nusu ya mavuno yao na hivyo kushindwa kuendelea na kilimo na sasa baadhi ya waliokuwa wameacha kulima, wameanza kurejea.

"Niliwahi kutunza magunia 300 lakini ambayo yalipona kuharibika yalikuwa 30, lakini kwenye hili ghala jipya ambalo tumejengewa, nilihifadhi magunia 300, yaliyoharibika ni mawili pekee na nilitunza kwa zaidi ya miezi sita," alisema Kumwenda.

Ofisa Tathimini na Ufuatiliaji wa Miradi kutoka Shirika la HELVETAS, Shoma Nangale, alisema walijenga ghala hilo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali pamoja na Chama cha Wakulima cha Igomelo AMCOS.

Alisema, mbali na kujenga ghala hilo, pia wanawasaidia wakulima kuwaunganisha na masoko ya uhakika kwa ajili ya kuuza mazao yao pamoja na kuwaunganisha na fursa zingine muhimu.

"Tunawawezesha pia wakulima kuzijua fursa zingine ambazo zipo kwenye kilimo kwa AMCOS, hii ya Igomelo tumewasaidia kwenye miundombinu na elimu," alisema Shoma.



## Wananchi waonywa utiririshaji majitaka

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISA Afya Baraza la Manispaa Wilaya ya Magharib 'B', Unguja amewataka wananchi kuchimba karo za kuhifadhi majitaka ili kuepusha kutitirisha ovyo maji machafu yanayosababisha maradhi.

Yussuf Mati Ali alitoa angalizo hilo jana alipozungumza na Nipashe ofisini kwake visiwani Zanzibar.

Alisema inasikitisha kuona zaidi ya asilimia 90 ya nyumba zilizoko katika manispaa hiyo hazina karo za kuhifadhi majitaka, hali inayochangia uchafuzi wa mazingira na kuhatarisha afya za wakazi wa maeneo hayo.

Yussuf alikumbusha kuwa Sheria Na. 11 ya Mwaka 2012 ya Afya ya Jamii na Mazingira, inamtaka kila mwananchi katika makazi yake aimarishe usafi.

Alisema sheria za nchi kuhusu masuala ya ardhi, pia zinamtaka kila mtu mwenye nyumba ahakikishe anajenga karo mbili, ikiwamo ya maji taka.

Alisema mtu yeyote ambaye hana karo ya majitaka, anaingia kwenye jinai kwa kuwa ameshindwa kudhibiti utiririshaji wa maji hayo yanayohatarisha afya za wananchi.

Alisema zipo baadhi ya nyumba katika wilaya hiyo zimejengewa karo za maji taka lakini karo hizo haziridhishi na hazikidhi vigezo na wakati vipindi vya mvua, majitaka hutoka kwenye karo hizo na kuenea katika maeneo ya makazi ya watu na kwenye vyanzo vya maji.

Alitumia fursa hiyo kusisitiza kwamba kila mwananchi anapoanza ujenzi ahakikishe anazingatia suala la karo ya maji taka ili kukidhi vigezo na kuepuka kuzuka kwa maradhi.

# Kilimo alizeti chapewa kipaumbele Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema serikali itaendekea kutoa elimu na kuhamasisha wakulima kuzalisha kilimo cha alizeti.

Alitoa kauli hiyo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi alipojibu swali la Mwakilishi wa Nafasi za Wanawake, Saada Ramadhan Mwenda.

Mwakilishi huyo alitaka kujua mpango wa serikali kuwahamasisha wakulima kujikita katika kilimo cha alizeti katika kukabiliana na uhaba wa mafuta.

Waziri Shamata alisema elimu hiyo itasadia kufanya kazi kwa mitambo miwili ya kuchakata zao hilo na hata kutumika kwa ufanisi.

"Tuna mitambo miwili, mmoja uko Pemba na mwingine Unguja kwa ajili ya kuchakata zao hilo na kupata mafuta," alifafanua.

Waziri huyo alisema katika miaka ya hivi karibuni kumejitokeza shida ya mabadiliko ya hali ya hewa na mvua nje ya msimu wa kawaida, hivyo kurudisha nyuma uzalishaji wa zao hilo.

Alisema kilimo cha alizeti hakihitaji mvua kubwa hasa pale zao hilo linapoanza kutoa maua.

Alibainisha kuwa jumla ya tani 137 za mafuta ya alizeti ziliingizwa Zanzibar katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita.



Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani nje ya mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wapewa mbinu za kukabili saratani

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MASHUJAA wa saratani kutoka Jema Foundation Tanzania wamewataka watu wanaougua ugonjwa huo, kuhakikisha wanafuata maelekezo ya madaktari katika matibabu na kuna uwezekano mkubwa wa kupona.

Walitoa rai hiyo jana walipowatembelea wagonjwa wa saratani waliolazwa katika Hospitali ya Mnazimmoja Zanzibar, wakisisitiza kuwa ufuasi wa masharti ya madaktari ni muhimu katika kuwezesha kupona ugonjwa huo.

Akizungumza na wagonjwa hao, mmoja wa mashujaa hao, Jema Mahmoud Baruan, alisema jambo la msingi kwa wagonjwa wa saratani ni kutovunjika moyo na kutoogopa, akisisitiza kuwa watu wengi wana dhana kuwa mtu ukishapata ugonjwa huo, huwezi kupona.

Jema ambaye ni mkuu wa taasisi hiyo na mwathirika wa saratani ya mitoki, alisema aligundulika kuwa na ugonjwa mnamo mwaka 2017 na kufanya tiba na alipona.

"Nilikuwa ninapitia madhila mbalimbali, lakini sikukata tamaa. Niliendelea na tiba na nimepona, hivyo na wenzetu mliopo mtapona, muhimu ni kufuata miongozo ya kitaalamu," alisema.

Jema alisema ikiwa watu watakuwa na utamaduni wa kupima afya mara kwa mara na watagundulika mapema kama wanaugua saratani na watapewa tiba na kupona kabisa.

Rosemary Chisanga aliyeugua saratani ya ngozi, alisema kuwa awali alikwenda hospitalini na kuambiwa kwamba ana shida na alipokwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili, aligundulika kuwa na saratani ya pili ya ngozi mwaka 2021.

Alisema kuwa katika kipindi chote cha matibabu yake, mapambano yalikuwa ni mengi na kupitia maumivu na mateso lakini alikubaliana na hali hiyo na kuzingatia matibabu na lishe bora na sasa amepona.

Stella Herman, shujaa wa saratani ya utumbo mpana, alisema aligundulika kuwa na ugonjwa huo mwaka 2020 na alipatiwa matibabu ya upasuaji, tiba ya dawa na mionzi 30 ya tumbo.

Mkurugenzi wa Hospitali Mnazimmoja, Dk. Marijani Msafiri Marijani, aliwapongeza mashujaa hao kwa kuwatembelea wenzao na kuwafariji wagonjwa walioko katika hospitali hiyo.

Alisema saratani ni ugonjwa sugu na wagonjwa wanakuwa katika maumivu makali na jambo kubwa wanalohitaji ni kupata ushirikiano kama huo kwa kuwapa moyo katika kupambana na maradhi hayo.

Dk. Marijani alibainisha kuwa kwa Zanzibar saratani zinazoongoza ni za matiti, tezi dume na shingo ya kizazi.

Alisema kwa mwaka 2021, wagonjwa wa saratani ya matiti walikuwa 57, saratani ya tezi dume wagonjwa 40 na wagonjwa 28 wa saratani ya shingo ya kizazi.

Alisema saratani ipo katika kundi la magonjwa ambayo siyo ya kuambukiza, hivyo ni vyema wananchi kubadilisha maisha yao kwa kufanya mazoezi, kupunguza uzito, kuacha kunywa pombe, kula vyakula vya mboga na matunda na kuacha kuvuta sigara.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**AMOSI JEREMIA MBOTOO** anatangaza kupotea kwa cheti cha darasa la saba chenye namba **PS 002** cha Shule ya Msingi **BAHI MAKULU** mwaka **2017.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/BAH/RB/598507/2021.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ASHA MOHAMEDI NANDILE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0523-0002** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NAMTUMBO SEKONDARI** mwaka 2011. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/360435/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMED HUSSEIN KALANJE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CROWN** yenye rangi ya PEARLY yenye usajili namba **T225 EAD,** CHASSIS NAMBA: **GRS2040005602** na ENGINE NAMBA:**2GR2825503.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/359121/2022**

## NYUMBA INAPANGISHWA

- Iko Masanga.Mjini Igunga
- Ina vyumba 5 vingine self-contained
- Ina Umeme na maji
- Ina eneo la kulima (Bustani)

**Mawasiliano**
**0756 767 070**
**Email:**
**smashindike@yahoo.com**

## NYUMBA INAPANGISHWA

- Iko Njiro,Mjini Arusha
- Ina vyumba 2 vya kulala ,Sebule, Stoo na Jiko.
- Ina umeme na maji

**Mawasiliano**
**0756 767 070**
**Email:**
**smashindike@yahoo.com**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOSEPH CANISIUS NDUNGURU** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili ***T 252 DLW – LANDROVER 110 DEFENDER.*** Chassis namba **SALLDHMFVA115764.** Engine namba **16L57978A.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/362445/2022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**KELVIN ROMAN METTA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S249-0025** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ALPHA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2010.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:DOD/DOD/RB/362097/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GOODLUCK P. EDWARD** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2809** cha **MALAMBO SEKONDARI mwaka 2017.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **114/17/02/2021.**

**KAPALAMA INTERNATIONAL LIMITED**
**P.O. Box 3257, Dar es salaam.**
**Cell: +255 758-536 060; +255 714 300 700,**
**Email address: kapalama2000@gmail.com**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na Dagaa Microfinance Ltd, tunauza kwa mnada dhamana ya ndugu Ndelilo Athanas Urio, ni gari aina ya Alhpad Toyota yenye usajili namba **T 351 DRB.** Mnada utafanyika tarehe 18/09/2022.

**Kwa mawasiliano Zaidi piga simu namba 0714 300 700.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KILINDI**

**MAOMBI MADOGO NA. 11 YA MWAKA 2022**
**LUSANE VILLAGE..................MSHINDA TUZO**
**DHIDI YA**
**CHARLES DALUSI..................... MSHINDWA TUZO NA.1**
**KWA MSHINDWA TUZO, CHARLES DALUSI,**

**POPOTE PALE ULIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**
Lusane village wameleta maombi dhidi yako mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) kilindi-Tanga lililopo Songe. Maombi haya yamepangwa kusikilizwa tarehe 22/09/2022 saa tatu asubuh mbele ya Mh.E.R Mhina Mwenyekiti.
Hivyo basi unatakiwa kufika wewe mwenyewe au wakili wako kwa tarehe iliyopangwa. Vielelezo kuhusu shauri hili vinapatikana katika masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Kilindi, Endapo hautatekeleza haya shauri hili litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Kilindi leo tarehe 12/09/2022

A.R. MWANKEJELA RESIDENT MAGISTRATE MANYONI
RESIDENT MAGISTRATE
MANYONI

**MHINA ER**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KILIDNI**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **RIDHAA JAFARI MBISI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **FEKON** yenye namba za usajili **MC 545 AGA.** Yenye Chassis Na. **LDAPAJOB9EGB15818** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi:**MUH/RB/2678/2022.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 97 OF 2022**

In the Matter of the Estate of the Late: **HERMAN ANDREA MOLLA**

**BY 1. BERTHA KIMATHI MOLLA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 28 day of SEPTEMBER.........2022

Dated at MOROGO this 12 day of SEPTEMBER.........2022

RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O. Box 660, Morogoro

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA NYUMBA NA ARDHI**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 48 YA 2022**

**CUTHBERT LEMWEL MSAKI (msimamizi wa mirathi ya marehemu: WILLIAM ELIBARIKI MACHA)......MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**NATIONAL MICROFINANCE BANK PLC, LJ INTERNATIONAL, ALEX ANTONY KIGODA, NA PRO. PHILBERT RWEHUMBIZA................{WAJIBU MAOMBI}**

**WITO KUITWA SHAURINI KWA**

**ALEX ANTONY KIGODA** popote ulipo unaarifiwa kufika katika baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro tarehe 16 mwezi wa 09 mwaka 2022 mbele ya Mwenyekiti E. Mogasa ww binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa MKONO wangu na MUHURI wa Baraza leo tarehe 08 mwezi 09,2022

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

**IN THE DISTRICT COURT OF GEITA**
**AT GEITA**
**MISC. CIVIL APPLICATION CASE NO. 23 OF 2021**

**MAYUNGA LUCAS**
**.....................................................................**
**...........APPLICANT/APPELANT/PETITIONER**

**VERSUS**

**MAHAKA KISHEPO NG'OMBE AND IZENGO KISHEPO.........................................DEFEN-DANT/ RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF HEARING/MENTION**

**TAKE NOTICE THAT,** the above case has been fixed for HEARING on the 15th day of SEPTEMBER, 2022 at 8.30 AM. In the forenoon.
YOU ARE required to appear in this court without fail and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
Given under my and the seal of the court this 12 day of SEPTEMBER, 2022

TO BE SERVED UPON:
PRINCIPAL/SENIOR/RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ZAKALIA SAIMON NYAISA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA HIACE.** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 237 CAM.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI **KAH /RB/ 618 /2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**NDUGU ROMANUS KAMOTE MLOWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Trekta yenye namba za usajili **T366AKJ** aina ya **SWARAJ.** Rangi Blue/White yenye Engine **No.6714035450657,** Chasis No. **QVTH45606105052.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu kwa kumbukumbu namba **DOD/DOD/RB/352014/2022**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**IN THE DISTRICT COURT (DISTRICT DELEGATE) OF MANYONI AT MANYONI**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.3/2022**
**In the matter of the Estate of the Late JOSEPH GAU MAKALA**
**And**
**In the matter of Application for Grant for letters of Administration by**
**LUSIA MICHAEL KILONGOZI ...... PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of probate and Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 26th Day of September,2022. Of the publication of this citation in the newspaper.
Dated at Manyoni this 5th day of September, 2022.

A.R. MWANKEJELA RESIDENT MAGISTRATE MANYONI
RESIDENT MAGISTRATE
MANYONI


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ENG: MR. GUO OBING**
MTAJWA HAPO JUU WA KAMPUNI YA UJENZI YA **CHINA & BRIDGE CORPORATION** (TANZANIA OFFICE) ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA MAGARI:

1. **REG.No.TZS 1262**
   CHASSIS No.**FV.413 P 500140,**
2. **T 252.AGY**
   CHASSIS No.**FV 415 J.43310.**

TAAARIFA IMETOLEWA POLISI KWA KUMB **No.MBE/MBE/RB/360259/2022**
**CONTROL No. 9910834248684**
Kwa Mwenye Taarifa yoyote anaweza kupeleka Kituo chochote cha Polisi kilichokaribu naye

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIETH M. CHRISTOPHER** anatangaza kupotelewa na Cheti cha form six chenye Index NO. **S0108-0660** kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia **IFUNDA TECHNICAL SECONDARY SHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/358156/2022.**

**RAMASHA COMPANY LIMITED**
**P.O BOX 1376 ARUSHA - TANZANIA**
**(UNDER LIQUIDATION)**

**AT AN EXTRA ORDINARY GENERAL MEETING OF THE MEMBERS OF THE COMPANY HELD AT THE REGISTERED OFFICE ON 1ST DAY OF AUGUST 2022**

**NOTICE OF FINAL WINDING UP MEETING**

1. **NOTICE** is hereby given to the general public for a final winding up meeting which will be hold on 5th August 2022 10:00am at **RAMASHA COMPANY LIMITED** offices.
2. The meeting is called by **MR. FAISAL SAMSON SALIM RUKAKA,** the liquidator of **RAMASHA COMPANY LIMITED,** we further notify the general public that;
   a. All shareholders and creditors of the company both secured and unsecured are required to attend this meeting.
   b. With effect from the publication of this Notice, no person is allowed to raise any claim against the company to the liquidator after this meeting.
   c. All legal and natural persons, who hold any property of the company, are required attend this meeting.

**IT IS HEREBY CERTIFIED** that the above was duly passed in accordance with and complied with the Memorandum and Articles of Association.
Dated this 1st day of August, 2022.

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mwili wa Malkia Elizabeth wawasili Scotland

**LONDON,** UINGEREZA

MWILI wa Malkia Elizabeth II umewasili mjini Edinburgh, Scotland ambako umelazwa katika makazi rasmi ya kifalme, kuwapa nafasi wafuasi na mashabiki wake kutoa heshima zao za mwisho.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na VOA, gari lililobeba mwili wa hayati Elizabeth, likiwa na maofisa wa kifalme na walinda usalama, liliondoka kwenye Kasri la Balmoral, ukiwa ni mwanzo wa safari ndefu na ya mwisho ya Malkia Elizabeth, aliyeaga dunia Alhamisi ya wiki iliyopita, baada ya kushikilia wadhifa wa ufalme wa Uingereza kwa miongo saba.

Msafara wake ulionekana kwa polepole ukipitia mabonde na milima ya Scotland na mandhari iliyothaminiwa na marehemu eneo ambapo alitumia wiki zake za mwisho za amani.

Katika miaka ya nyuma, malkia alionekana mara kwa mara akitembelea vijiji hivyo vya mbali, alipokuwa akiishi katika Kasri la Balmoral, makao ambayo aliyapenda.

Wakazi walikusanyika kando ya barabara ili kumtazama kwa mara ya mwisho na kusema kwaheri.

Wengine walitulia na kuonyesha ukimya ambao ulikuwa ni ishara ya mshtuko ambao raia wa Uingereza walipata na heshima ambayo marehemu alipewa wakati wa uhai wake.

Baadhi ya watu walirusha maua, huku wengine wakipiga vigelegele wakati gari la kubebea maiti lilipopita, pamoja na wengi wao katika umati wakibubujikwa na machozi. **VOA**





Rais Uhuru Kenyatta akimkaribisha William Ruto na mkewe Ikulu. **PICHA: TKN**

# Macho yote kwa Kenyatta akikabidhi kiti kwa Ruto leo

**NAIROBI,** KENYA

RAIS mteule wa Kenya William Ruto, anatarajia kuapishwa leo, huku macho na masikio yote yakiangazia hotuba atakayoitoa Rais Uhuru Kenyatta.

Aidha, Rais mteule Ruto ametoa mwanga wa agenda ya sera yake ya mambo ya nje, akiahidi kuchangia masuala muhimu ya Afrika Mashariki, kudumisha amani na kuongeza mchango wa nchi hiyo katika juhudi za usalama wa kikanda.

Ruto aliyabainisha hayo katika mahojiano aliyofanya na kituo cha televisheni cha Marekani CNN wiki iliyopita.

Dk. Ruto, ambaye anatarajiwa kuapishwa leo, hakudokeza chochote kuhusu mabadiliko yoyote makubwa ya sera ya mambo ya nje kutoka ile ya mtangulizi wake Uhuru Kenyatta, huku sherehe za kuapishwa kwake zikitarajiwa kufanyika katika uwanja wa michezo wa Kasarani mjini Nairobi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na VOA, Dk. Ruto anachukua kiti cha kuiongoza Kenya huku kukiwa na changamoto na fursa nyingi nchi humo, kikanda na eneo kubwa la Pembe ya Afrika.

Inaelezwa kuwa Ruto anaweza kutumia mafanikio ya kidiplomasia ya mtangulizi wake Uhuru Kenyatta yaliyofanyika katika mwingiliano wa kikanda na kuiweka Kenya katikati ya amani ya kikanda na miradi ya kiusalama, au kuamua kufuata njia yake mwenyewe kwa kutumia fagio jipya la kisiasa na kiuchumi.

Katika ilani yake ya kisiasa, Dk. Ruto alisema chama chake cha Kenya Kwanza Alliance kina nia ya dhati kwa mwingiliano wa kikanda ambao utaifanya Kenya kituo muhimu katika kanda hiyo.

Ilani ya chama cha Rais mteule inaeleza katika kifungu cha sera ya mambo ya nje kwamba itaendelea kuimarisha ahadi zao kwa jumuiya ya kimataifa.

"Serikali ya Kenya Kwanza itahakikisha kuwa nchi inaheshiwa na kuthaminiwa kote ulimwenguni. Itahamasisha mahusiano ya kirafiki na jirani zake, itachukua nafasi ya mbele katika masuala ya kikanda na barani Afrika, itashirikiana na washirika wake wa kimataifa," ilisema.

> **Moja ni kwamba nitakuwa nimeacha jamii iliyoungana, yenye mshikamano, na pili, tutakuwa tumeshinda vita dhidi ya ufisadi.**

Pia ilielezwa kuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) bado ni changamoto, wakati Uhuru alipokuwa amefuata sera ya kupunguza vita upande wa mashariki mwa DRC, ambapo Dk. Ruto anaanza kutoa hatua isiyotabirika katika mahusiano yake na nchi ya pili kubwa barani Afrika na kiongozi wake, Felix Tshisekedi.

Taarifa hiyo ilisema Rais Kenyatta alikuwa kati ya viongozi wachache wa Afrika waliohudhuria kuapishwa kwa Rais Tshisekedi mjini Kinshasa wakati viongozi wengine wa Afrika na Umoja wa Afrika (AU), walikuwa na shaka kuhusu ushindi wake dhidi ya Martin Fayulu.

Hivi karibuni Rais Kenyatta alikuwa mwenyeji wa wakuu wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kujadili kuzorota kwa usalama huko mashariki mwa DRC na kufanya bidii kuundwa kwa Kikosi cha Dharura cha Afrika Mashariki, na upelekaji wa wanajeshi nchini DRC.

Pia aliweka nia ya dhati ya kutuliza hali ilivyo huko mashariki mwa DRC kwa kupeleka wanajeshi 200 wa Jeshi la Ulinzi la Kenya (KDF) kukabiliana na wanamgambo wanaosababisha vurugu kwa raia na kutishia uwepo wa walinda amani wa Umoja wa Mataifa.

### KENYATTA AMKARIBISHA RUTO IKULU

Rais anayeondoka Uhuru Kenyatta alikutana na Rais mteule William Ruto katika Ikulu ya Nairobi, ambapo Uhuru na mkewe Mama Margaret Kenyatta waliwakaribisha Ruto na Mama Rachael jana alasiri katika Ikulu hiyo ya Nairobi.

Naye Rais katika kikao na wajumbe wa Azimio alisema kuwa licha ya kwamba chaguo lake halikufaulu kuingia Ikulu, Baba ndiye atasalia kuwa kiongozi wake.

"Nitapeana upanga huku nikiwa natabasamu kwa sababu ni jukumu langu kikatiba, lakini mimi kiongozi wangu atasalia kuwa Baba," alisema Uhuru.

### KENYATTA ATAKUMBUKWA VIPI

Mwanafunzi mmoja alipomuuliza Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta mwaka wa 2018 kuhusu jinsi ambavyo angependa kukumbukwa atakapoondoka madarakani, alionekana kufurahishwa na swali hilo, kabla ya kutaja mambo mawili.

"Moja ni kwamba nitakuwa nimeacha jamii iliyoungana, yenye mshikamano, na pili, tutakuwa tumeshinda vita dhidi ya ufisadi," alisema.

Miongoni mwa maswali yanaoulizwa ni anapojiandaa kuachia ngazi baada ya mihula miwili na kukabidhi madaraka mshirika wake wa zamani aliyegeuka kuwa mpinzani wake William Ruto, je, amefikia malengo hayo na mengine.

Hatua muhimu zaidi kuelekea umoja wa kitaifa ilikuwa Machi 2018 alipopeana mkono na kiongozi wa upinzani na aliyekuwa Waziri Mkuu Raila Odinga kama ishara ya mapatano yao ya kisiasa.

Kupeana mkono kulimaliza miezi kadhaa ya sintofahamu na machafuko kutokana na uchaguzi ambao ulibatilishwa na Mahakama ya Juu 2017, na uchaguzi wa marudio unadaiwa kususiwa na Odinga, ambaye aliendesha sherehe yake ya kuapishwa katika mji mkuu Nairobi.

Lakini mapatano ya Kenyatta na Odinga hayakupokelewa vyema na Naibu Rais William Ruto, ambaye alidai kwamba yalivuruga ajenda yao madhubuti ya kuimarisha usalama wa chakula, kufikia huduma ya afya kwa wote, kujenga nyumba za gharama nafuu zaidi na kukuza sekta ya viwanda.

Hili hatimaye lilisababisha wawili hao kutofautiana, huku Kenyatta akiondoa uungaji mkono wake kwa Ruto na badala yake kumuunga mkono mpinzani wake Odinga, katika kuwania urais katika uchaguzi wa Agosti mwaka huu.

Mvutano kati ya Kenyatta na naibu wake ulitajwa kuendelea hata baada ya uchaguzi na kwamba bado hajatoa pongezi hadharani kwa Ruto juu ya ushindi wake, ingawa alisema atafanikisha mabadiliko ya mamlaka kwa njia ya amani. **VOA/BBC**

# MINZIRO ALIA KUPOTEZA NAFASI CAF, LYANGA AAHIDI MABAO DAR

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Hilal Alsahil ya Sudan ikiwa ugenini juzi, Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro amesema vijana wake walipoteza nafasi nyingi za kufunga mabao kutokana na kukosekana kwa umakini na utulivu, huku nadhodha wa kikosi hicho, Daniel Lyanga akiahidi kufanya vema kwenye mechi ya marudiano wiki ijayo nchini Tanzania.

Akizungumza baada ya mechi hiyo ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika, iliyoingia kwenye rekodi ya kuwa mechi ya kwanza ya kimataifa kwa Geita Gold tangu kuanzishwa kwake, Minziro alisema ilikuwa ya ushindani, lakini wao walitawala mchezo kwa kiasi kikubwa, ila kilichokosekana ni umakini na utulivu wa wachezaji wake kupachika mpira ndani ya wavu, lakini akaahidi kuendelea kulifanyia kazi mazoezini.

**“Mechi ilkuwa na ushindani, ingawa walicheza nyumbani, lakini sisi tulipoteza nafasi nyingi kuliko wao, ni kweli tumemkosa George Mpole, lakini kama hawa waliobaki wangekuwa makini na utulivu tungetoka na ushindi.**

“Hii ni shida kubwa kwa vijana wetu, si hawa wangu wa Geita Gold tu, hili ni tatizo la wachezaji wengi wa Kitanzania, wanakuwa hawana utulivu na umakini wanapoingia kwenye eneo la hatari la timu pinzani,” Minziro alisema.

“Hata mazoezini huwa nasisitiza utulivu, vijana hawa wakiwa watulivu ipo siku kuna timu itachukua mabao matatu mpaka matano kutokana na nafasi nyingi tunazotengeneza.”

Nahodha wa kikosi hicho, Lyanga aliahidi mazuri kwenye mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa Jumamosi wiki hii kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

“Mchezo unaofuata tunaahidi mazuri, kwenye mechi hii tuliutawala mchezo kwa dakika zote 90, hata bao lao lilikuwa la piga nikupige tu, halikuwa la kutengenezwa, sisi tumekosa nafasi saba za wazi,” alisema Lyanga.




Ofisa Mkuu Rasilimali Watu wa Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay (wa pili kushoto), akionyesha zawadi zitakazotolewa kwa washindi wa NMB Marathon 2022, jijini Dar es Salaam jana. Mbio hizo zitakazofanyika Septemba 24, zitaanzia na kuishia kwenye viwanja vya Leaders Kinondoni, Dar es Salaam. Kushoto ni Mratibu wa NMB Marathon, David Marealle na kulia ni Mkurugenzi wa Ufundi wa mbizo hizo, Suleiman Nyambui. **MPIGAPICHA WETU**

# *Bingwa NMB Marathon kulamba mil. 3/-*

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mbio za NMB Marathon zikitarajiwa kufanyika Septemba 24, mwaka huu, imefahamika kuwa mshindi wa mbio hizo kwa kilomita 21, anatarajiwa kuondoka na kitita cha Sh. milioni tatu.

Hayo yalisemwa jana na Ofisa Mkuu Rasilimali Watu NMB, Emmanuel Akonaay, wakati akitangaza zawadi za washindi mbalimbali za marathon hizo ambazo huu ni msimu wake wa pili kufanyika lengo lake likiwa ni kukusanya kiasi cha Sh. milioni 600 kwa ajili ya kusaidia matibabu ya kinamama wenye ugonjwa wa fistula katika Hospitali ya CCBRT.

Mbio hizo zenye kaulimbiu ya ‘Mwendo wa Upendo’, zinatarajiwa kufanyika katika viwanja vya Leaders vilivyopo Kinondoni, Dar es Salaam.

Akonaay alisema: “Kwa mshindi wa kwanza kwa kilomita 21 kwa wanawake na wanaume watapata milioni tatu kila mmoja, wa pili milioni 1.8, watatu Sh. 800,000, wa nne Sh. 600,000 huku wa tano akipata Sh. 350,000 na wa sita Sh. 250,000.

“Kwa upande wa kilomita 10, wa kwanza ataibuka na Sh. milioni moja kwa wanaume na wanawake, wa pili laki Sh. 800,000, wa tatu Sh. 500,000, wa nne Sh. 300,000, wa tano Sh. 200,000 na wa sita Sh. 150,000 huku kwa upande wa kilomita tano (kwa watoto) wa kwanza akizawadiwa baiskeli yenye thamani ya Sh. 600,000, wa pili vocha ya Sh. 200,000 na watatu ‘smart watch’ ya Sh. 200,000.

“Tunawaomba watu wote wenye nia njema waungane na sisi ili tuweze kufikia azma ya kutimiza kiasi hiki cha Sh. milioni 600,” alisema Akonaay.

Kwa upande wa Mratibu wa mbio hizo, David Marealle, alisema: “Mwamko ni mkubwa kwa wale ambao wanaendelea kujiandikisha kwa ajili ya kushiriki mbio hizi ambapo vituo vyetu vinaendelea kuandikisha watu.

“Tutakuwa na siku tatu kwa ajili ya watu kuchukua vifaa zikiwamo namba na ‘tsheti’ baada ya kujiandikisha ambazo ni Septemba 21, 22 na 23,” alihitimisha Marealle.

Naye Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Riadha, Seleman Nyambui, alisema: “Hadi sasa maandalizi yanaendelea vizuri kabisa na uzuri ni kuwa NMB Marathon kila mwaka huwa na jambo tofauti, hivyo na mwaka huu watakuja nalo.

“Mara nyingi ilizoeleka kuona washindi watatu wa juu pekee ndiyo ambao wanapewa zawadi, lakini mara hii imekuwa tofauti kabisa na sisi tutahakikisha washindi wa haki wanapatikana kabisa, hakutakuwa na wale ambao watakatisha njia ili washinde,” alisema.

# Prisons yamwagiwa mamilioni ya udhamini

**Na Saada Akida**

KLABU ya Tanzania Prisons, imeingia mkataba wa mwaka mmoja wa udhamini na Kampuni ya kimataifa ya usafirishaji mizigo kutoka mataifa mbalimbali kuja nchini (Silent Ocean), wenye thamani zaidi ya Sh. milioni 50.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Tanzania Prisons, Enock Mwanguku, aliishukuru Kampuni ya Silent Ocean kwa kuiamini Tanzania Prisons kuwa sehemu ya wao kutangaza biashara yao ili kufikia wadau wengi zaidi kibiashara.

“Tunashukuru kampuni hiyo kwa kuamua kuwekeza kwenye timu yetu kwa sababu kuna klabu nyingi wengeweza kuwekeza huko, lakini wamekuwa na imani na Tanzania Prisons, tunawahakikishia hatutawaangusha.

“Hizi fedha zitaenda kuimarisha zaidi baadhi ya maeneo katika timu yetu ikiwamo suala la mishahara na kusaidia kusafiri kwa timu kwenda sehemu ya kituo cha mechi,” alisema Mwanguku.

Alisema udhamini huo utaleta chachu ya kujiandaa kwa timu yao kufanya vizuri katika michezo iliyopo mbele yao ikiwamo kutocheza kwa presha kubwa mwisho wa msimu.

Naye Mkuu wa Idara ya Mauzo na Masoko wa Silent Ocean, Mohammed Kamilagwa (pichani chini), alisema lengo kubwa la kampuni hiyo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kuendeleza michezo ambayo imekuwa sekta inayotoa ajira kwa vijana wengi.

“Kama Kampuni ya Silent Ocean, tuna jukumu la kurudisha kwa jamii kidogo tunachokipata na tumechagua kuiwezesha timu ya Jeshi la Magereza, Tanzania Prisons, hii ni taasisi ya serikali,” alisema Kamilagwa.

Alisema lengo ni kuifanya iweze kushindana na kufanya vizuri kwenye mashindano yote, na wanaamini Tanzania Prisons imefanya usajili mzuri na kuanza kufanya vizuri msimu huu wa ligi.



## ZISIKUPITE

### BAYERN YAMKANA KANE

MKURUGENZI wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amekanusha madai ya kufanya mazungumzo ya kutaka kumsaili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29. ***(Sport1 via Goal)***

### DE JONG SASA KUUZWA

BARCELONA itajaribu tena kumuuza kiungo wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la Januari baada ya kushindwa kumuuza dirisha lililopita la majira ya joto kwenda Manchester United. ***(Forbes via 90min.com)***

### NEWCASTLE NA KARIUS

KLABU ya Newcastle United imesitisha kwa muda kutangaza rasmi usajili wa golikipa, Loris Karius, 29, kwa sababu ya kuheshimu kifo cha Malkia Elizabeth II. ***(Northern Echo)***

### UNITED YAMFUNGUKIA DEPAY

KLABU ya Manchester United ilikataa nafasi ya kumsajili tena straika wa Uholanzi, Memphis Depay, 28, kutoka Barcelona. ***(Fabrizio Romano - YouTube)***

### RONALDO KUONDOKA JANUARI

WACHEZAJI wa Manchester United wanaamini fowadi wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, bado anataka kuondoka Old Trafford na atalazimisha Januari. ***(Sun)***

### SANGARE NI UNITED, LIVER

LIVERPOOL inapanga kuingia kwenye mbio moja na Manchester United kuwania saini ya kiungo wa PSV Eindhoven, Ibrahim Sangare mwenye umri wa miaka 24, ambaye amekuwa akiwaniwa pia na West Ham, Leicester City na AC Milan. ***(Calciomercato via Express)***

### LEAO ANUKIA CHELSEA

NAFASI ya Chelsea kumsajili, Rafael Leao imeongezeka baada ya winga huyo mwenye umri wa miaka 23, mazungumzo yake kuhusu mkataba mpya na AC Milan kusimama. ***(Corriere dello Sport via Mail)***

### POSTECOGLOU KUMRITHI POTTER

KOCHA wa Celtic, Ange Postecoglou mwenye umri wa miaka 57, ni moja ya majina yanayotajwa kumrithi Graham Potter kule Brighton. ***(Times)***

### LUIZ ANANYATIWA LIVER

KIUNGO wa Aston Villa, Douglas Luiz, 24, pia ananyatiwa na Liverpool, ambao watajiandaa kumtoa Alex Oxlade-Chamberlain, 29. ***(Express)***

### MCKENNA HAITAKI BRIGHTON

KOCHA wa Ipswich City, Kieran McKenna mwenye umri wa miaka 36, amesema malengo yake kwa sasa ni kuhakikisha timu yake inapanda daraja, licha ya kuhusishwa na Brighton. ***(Manchester Evening News)***

### CARROLL KUTUA READING

STRAIKA Andy Carroll, 33, ambaye ni mchezaji huru kwa sasa, anapanga kujiunga na Reading inayocheza Championship. ***(Reading Chronicle)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL AVUNJA UKIMYA KUTIMULIWA CHELSEA

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amefichua kusikitishwa kwake na uamuzi wa Chelsea kumtimua mapema wiki iliyopita.

**Baada ya kuanza kwa kusuasua, mchezo wa mwisho wa Tuchel kuwanoa 'The Blues' hao ulikuwa ni kipigo cha bao 1-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Dinamo Zagreb Jumanne iliyopita.**

Matokeo hayo yakamfanya mmiliki kiongozi wa klabu hiyo, Tom Boehly kuamua kufanya mabadiliko ya benchi la ufundi kwa kumtimua Tuchel.

Graham Pottter aliteuliwa haraka kwa mkataba wa miaka mitano Alhamisi baada ya Chelsea kukubali kumnunua Muingereza huyo kutoka katika mkataba wake na Klabu ya Brighton.

Na Tuchel, ambaye aliiongoza miamba hiyo ya London kunyakua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, Super Cup na Klabu Bingwa Dunia, sasa amevunja ukimya kuhusu kuondoka kwake ghafla.

Raia huyo wa Ujerumani aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter: "Hii ni moja ya taarifa ngumu zaidi ambayo nimewahi kuandika na ni moja ambayo nilitarajia nisingehitaji kufanya kwa miaka mingi.

"Nimehuzunika sana kwamba muda wangu Chelsea umefikia kikomo. Hii ni klabu ambayo nilihisi niko nyumbani, kikazi na kibinafsi.

> ●●● Hii ni moja ya taarifa ngumu zaidi ambayo nimewahi kuandika, nimehuzunika sana...

"Asante sana kwa wafanyakazi wote, wachezaji na wafuasi kwa kunifanya nijisikie nimekaribishwa sana tangu mwanzo.

"Fahari na furaha niliyokuwa nayo kwa kuisaidia timu kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Klabu Bingwa Dunia itabaki nami milele.

"Nina heshima kuwa sehemu ya historia ya klabu hii na kumbukumbu za miezi 19 iliyopita zitakuwa na nafasi maalum moyoni mwangu."

Tuchel mwenye umri wa miaka 49, alichukua nafasi ya gwiji wa Chelsea, Frank Lampard kwenye dimba la Stamford Bridge, Januari mwaka jana.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,031,2

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 14 NA 15 SEPTEMBA 2022

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 14/09/22 | 19:45 | Shakhtar Donetsk vs Celtic | 3.05 | 3.50 | 2.24 |
| 02. 14/09/22 | 22:30 | Colon Santa Fe vs San Lorenzo | 2.32 | 2.99 | 2.99 |
| 03. 15/09/22 | 00:00 | Everton Vina del Mar vs Nublense | 2.29 | 3.04 | 2.99 |
| 04. 15/09/22 | 03:05 | Alebrijes De Oaxaca vs CF Atlante | 2.89 | 3.09 | 2.32 |
| 05. 15/09/22 | 03:30 | Lanus vs Boca Juniors | 2.85 | 2.99 | 2.41 |
| 06. 15/09/22 | 05:00 | Vancouver Whitecaps vs LA Galaxy | 2.52 | 3.61 | 2.59 |
| 07. 15/09/22 | 19:45 | Olympiakos vs SC Freiburg | 2.58 | 3.39 | 2.58 |
| 08. 15/09/22 | 19:45 | Karabakh vs Nantes | 2.54 | 3.30 | 2.69 |
| 09. 15/09/22 | 19:45 | Djurgardens IF vs Molde | 2.40 | 3.30 | 2.86 |
| 10. 15/09/22 | 22:00 | Basaksehir vs Fiorentina | 2.73 | 3.28 | 2.51 |
| 11. 15/09/22 | 22:00 | Steaua Bucuresti vs Anderlecht | 2.72 | 3.32 | 2.50 |
| 12. 15/09/22 | 22:00 | Rigas Futbola Skola vs Hearts | 2.68 | 3.24 | 2.58 |
| 13. 15/09/22 | 22:00 | Partizan vs Nice | 2.72 | 3.37 | 2.47 |

KUWEKA PESA:

- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa · vodacom m-pesa · airtel money · ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa

SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# ANCELOTTI: NAJUA ASENSIO ANA HASIRA KUKAA BENCHI

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema, anamhurumia Marco Asensio baada ya hasira yake ya kuachwa kwenye benchi wakati Real Madrid ikishinda mabao 4-1 dhidi ya Mallorca, Jumapili.


'Los Blancos' walirejea kwenye kilele cha LaLiga baada ya kutoka nyuma na kudumisha ubora wa mwanzo wao wa msimu kwa asilimia 100, huku wakibaki kuwa timu pekee kwenye Ligi Kuu tano za Ulaya ambayo imeshinda mechi zake zote.

Juhudi nzuri za Federico Valverde zilisawazisha bao la mapema la Vedat Muqiri, huku mabao ya Vinicius Junior, Rodrygo na Antonio Rudiger yakikamilisha ushindi huo.

Asensio, ambaye mara kwa mara alihusishwa na kutaka kuondoka Santiago Bernabeu wakati wa dirisha la usajili, ameichezea Madrid kwa dakika 17 tu katika mashindano yote msimu huu.

Alipoulizwa kuhusu tukio hilo, Muitaliano huyo alisema: "Tulikuwa tunajiandaa ikiwa hatutafanya 2-1 kuwaweka Mariano na Asensio. Lucas ameumia, na tulikuwa na chaguo moja tu, na sikufikiria juu yake.

"Kama ana hasira nakubaliana naye ni jambo la kawaida, ina maana anataka kucheza, anajiona wa muhimu, katika kipindi hiki amekuwa mchezaji aliyeathirika zaidi kikosini na nazingatia hilo, nakubaliana na hasira zake."



## Eriksen: Manchester United ipo kwenye njia nzuri

**MANCHESTER,** England

CHRISTIAN Eriksen ana uhakika Manchester United wako kwenye "njia nzuri" na amesifu viungo wenzake wa kati wa 'Mashetani Wekundu' hao.

Ingawa United walipoteza kwa Real Sociedad kwenye Ligi ya Europa Alhamisi iliyopita, mafanikio yao ya Ligi Kuu England yameonekana kuimarika tangu Erik ten Hag alipopoteza michezo yake miwili ya mwanzoni mwa mwezi uliopita.

Ushindi wa mabao 3-1 nyumbani dhidi ya Arsenal Jumapili iliyopita ulifanya United kushinda mara nne mfululizo kwenye ligi.

Eriksen aliitengenezea timu nafasi tatu za juu na kuandikisha pasi 33 za mafanikio (pia za juu kwa timu) dhidi ya 'Washika-bunduki' hao, pamoja na kutengeneza bao la pili la Marcus Rashford.

Ni Diogo Dalot na Bruno Fernandes pekee (wote 10) wametengeneza nafasi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu kuliko Eriksen kwa United msimu huu (nane).

Akizungumza na tovuti ya klabu hiyo, Eriksen alisema viungo wa United walikuwa wakizoea mbinu za bosi huyo mpya.

## HABARI MICHEZO

43,893/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 17/09/22 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.73 | 3.33 | 2.48 |
| 02. 17/09/22 | 19:00 | Spezia vs Sampdoria | 2.55 | 3.25 | 2.75 |
| 03. 17/09/22 | 19:15 | Zulte Waregem vs St. Truiden | 2.94 | 3.49 | 2.28 |
| 04. 17/09/22 | 19:30 | Valencia vs Celta Vigo | 2.35 | 3.08 | 3.18 |
| 05. 17/09/22 | 19:30 | Borussia Monchengladbach vs RB Leipzig | 2.93 | 3.57 | 2.23 |
| 06. 17/09/22 | 20:00 | PAU F vs Valenciennes | 2.72 | 3.07 | 2.77 |
| 07. 17/09/22 | 20:00 | Bastia vs Metz | 2.52 | 3.17 | 2.92 |
| 08. 17/09/22 | 20:00 | US Quevilly Rouen vs Laval | 2.47 | 3.16 | 3.01 |
| 09. 17/09/22 | 22:30 | Atlanta United vs Philadelphia Union | 2.30 | 3.61 | 2.91 |
| 10. 18/09/22 | 02:30 | New England Revolution vs Montreal Impact | 2.35 | 3.57 | 2.87 |
| 11. 18/09/22 | 13:15 | GO Ahead Eagles vs FC Emmen | 2.36 | 3.48 | 2.83 |
| 12. 18/09/22 | 14:30 | Jahn Regensburg vs St. Pauli | 2.88 | 3.62 | 2.26 |
| 13. 18/09/22 | 15:00 | Randers FC vs Silkeborg IF | 2.47 | 3.39 | 2.74 |
| 14. 18/09/22 | 15:30 | SC Heerenveen vs Twente | 2.73 | 3.58 | 2.38 |
| 15. 18/09/22 | 16:00 | Clermont Foot vs Troyes | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 16. 18/09/22 | 17:30 | FC Arouca vs Vitoria Guimaraes | 2.79 | 3.19 | 2.54 |
| 17. 18/09/22 | 19:00 | FC Midtjylland vs FC Copenhagen | 2.50 | 3.40 | 2.70 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 13/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4952 | Gyeongnam vs Gimpo Citizen | 1.57 | 3.89 | 4.82 |
| 13:30 | 2562 | Busan I Park vs Daejeon Citizen | 3.79 | 3.45 | 1.83 |
| 13:30 | 4528 | Jeju Utd vs Daegu | 2.07 | 3.39 | 3.10 |
| 13:30 | 5295 | FC Seoul vs Gangwon | 2.03 | 3.39 | 3.19 |
| 14:00 | 1398 | Song Lam Nghe AN vs SHB DA Nang | 2.46 | 3.30 | 2.56 |
| 14:30 | 3689 | Guangzhou RF vs Guangzhou Evergrande | 2.41 | 3.35 | 2.75 |
| 15:00 | 3940 | Nizhny Novgorod vs FK Khimki | 1.79 | 3.40 | 4.04 |
| 16:00 | 5235 | Mbeya City vs Azam | 3.35 | 2.80 | 2.38 |
| 17:15 | 2401 | Kheybar Khorramabad FC vs Mes Shahr-e Babak | 1.71 | 2.99 | 5.49 |
| 17:30 | 1323 | Dinamo Moscow vs Akhmat Grozny | 1.63 | 3.73 | 4.61 |
| 17:45 | 2688 | Pars Jonoubi Jam vs Saipa Karadj | 2.55 | 2.70 | 3.10 |
| 18:00 | 5824 | Esteghlal Mollasani vs Shams Azar Qazvin | 2.18 | 2.76 | 3.60 |
| 18:05 | 2806 | Lekhwiya SC vs Al-Sailiya SC | 1.44 | 4.61 | 5.29 |
| 18:25 | 3951 | AL Sahel SC vs Alshoulla | 2.75 | 2.85 | 2.75 |
| 18:30 | 2202 | AS Douanes Ouagadougou vs AS Real Bamako | 3.48 | 3.28 | 1.97 |
| 18:30 | 2751 | Al Hala Muharraq vs AL Badii | 2.12 | 3.14 | 3.24 |
| 19:00 | 3937 | Young Africans vs Mtibwa Sugar | 1.30 | 4.42 | 9.82 |
| 19:45 | 2664 | Viktoria Plzen vs Inter | 6.79 | 4.70 | 1.39 |
| 19:45 | 2863 | Sporting Lisbon vs Tottenham | 3.51 | 3.46 | 1.98 |
| 20:00 | 2738 | Norrby IF vs Halmstads BK | 3.45 | 3.45 | 2.08 |
| 20:00 | 5321 | AFC Eskilstuna vs IK Brage | 2.54 | 3.56 | 2.60 |
| 20:15 | 2018 | Umm-Salal SC vs Al Arabi Doha SC | 3.29 | 3.43 | 1.98 |
| 21:30 | 1818 | Danubio FC vs Plaza Colonia CD | 1.85 | 3.04 | 4.32 |
| 21:45 | 1066 | Derry City vs Sligo Rovers | 1.61 | 3.55 | 5.12 |
| 21:45 | 1899 | Hull City vs Stoke City | 2.89 | 3.19 | 2.38 |
| 21:45 | 2257 | Cheltenham vs Cambridge Utd | 2.48 | 3.32 | 2.66 |
| 21:45 | 2473 | Blackburn vs Watford | 2.85 | 3.21 | 2.39 |
| 21:45 | 2482 | Huddersfield vs Wigan | 2.57 | 3.17 | 2.67 |
| 21:45 | 2730 | Charlton vs Forest Green | 1.84 | 3.59 | 3.89 |
| 21:45 | 2824 | Wycombe vs Accrington | 1.97 | 3.45 | 3.55 |
| 21:45 | 3162 | Barnet vs Dorking Wanderers | 2.13 | 3.54 | 2.99 |
| 21:45 | 3430 | Burton vs Portsmouth | 3.80 | 3.60 | 1.86 |
| 21:45 | 4236 | Barnsley vs Port Vale | 2.05 | 3.25 | 3.50 |
| 21:45 | 4393 | Shrewsbury vs Exeter | 2.81 | 3.11 | 2.49 |
| 21:45 | 4434 | Harrogate vs Salford City | 3.04 | 3.29 | 2.23 |
| 21:45 | 4982 | MK Dons vs Bolton | 2.54 | 3.19 | 2.69 |
| 21:45 | 5012 | Swansea vs Sheffield Utd | 3.20 | 3.30 | 2.16 |
| 21:45 | 5052 | Ipswich vs Bristol Rovers | 1.43 | 4.30 | 6.79 |
| 21:45 | 5233 | Halifax vs Gateshead | 2.10 | 3.44 | 3.14 |
| 21:45 | 5518 | Morecambe vs Sheffield Wed | 5.80 | 4.00 | 1.52 |
| 21:45 | 5735 | Peterborough vs Fleetwood Town | 1.65 | 3.85 | 4.69 |
| 21:45 | 5820 | Plymouth vs Oxford Utd | 2.22 | 3.30 | 3.05 |
| 21:45 | 5938 | Middlesbrough vs Cardiff | 1.69 | 3.50 | 4.91 |
| 22:00 | 1404 | Liverpool vs Ajax | 1.50 | 4.70 | 5.00 |
| 22:00 | 1783 | Bayern Munchen vs Barcelona | 1.75 | 4.20 | 3.70 |
| 22:00 | 2309 | Marseille vs Eintracht Frankfurt | 1.89 | 3.54 | 3.74 |
| 22:00 | 3535 | Porto vs Brugge | 1.38 | 4.59 | 7.38 |
| 22:00 | 3826 | Bayer Leverkusen vs Atletico Madrid | 2.80 | 3.30 | 2.39 |
| 22:00 | 4449 | Preston vs Burnley | 2.90 | 3.15 | 2.39 |
| 22:30 | 5668 | Velez Sarsfield vs Central Cordoba | 1.72 | 3.43 | 4.42 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SAMIA APONGEZA MABORESHO UWANJA MAJALIWA RUANGWA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akiwapongeza wananchi wa Ruangwa kwa kufanikiwa kuwa na uwanja wa kisasa wa Majaliwa uliofunguliwa juzi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ametaja sababu za dimba hilo kuwa la nyasi bandia na si za asili.

**Akizungumza kwenye uzinduzi wa uwanja huo, Waziri Mkuu alisema waliamua kuweka nyasi bandia kwa sababu eneo hilo lina maji ya chumvi chumvi iliyochangayika na magadi, hivyo nyasi asili zilikuwa hazistawi inavyotakiwa kwa wakati wote.**

Wakati uzinduzi huo unaendelea, Rais Samia alimpigia simu Waziri Mkuu akitaka kuongea na mashabiki waliojazana uwanjani hapo na aliwapongeza, akisema uwanja huo si tu kama utabadilisha soka la Mkoa wa Lindi, bali Tanzania nzima.

"Nawapongeza wana Ruwangwa kwa kuwa na uwanja mzuri sana, ambao utabadilisha soka la Tanzania kwani utazifanya timu zote kufanya mazoezi, hongereni na sherehekeeni kwa salama," alisema Rais Samia, huku akishangiliwa na mashabiki waliofurika uwanjani hapo.

Kwa upande wa Majaliwa, alikumbushia mchakato mzima hadi kujengwa wa uwanja huo ambao mwanzo ulikuwa wa nyasi asili, lakini kutokana na eneo hilo kuwa na maji chumvi, ilibidi wabadilishe na kuwa nyasi bandia.

"Natambua mchakato wa uwanja huu ulitokana na mawazo na matamanio yenu, mwisho mkaupata, hapa kulikuwa na mikorosho mingi, mlitafuta katapira chini ya halmashauri tukaiondoa, tukanunua nyasi za asili na mbegu zake tukapanda hapa, kutokana na maji ya eneo hili kuwa si mazuri kuwa na chumvi chumvi na magadi, tukaona nyasi haziwezi kufanya uwanja huu kutumika wakati wote. Wanaruangwa kwa kweli sina cha kusema, nimefurahi na nashukuru kwa kiasi ambacho siwezi kusimulia, baadhi yenu mkatoa mawazo ya kuchangia mlichonacho na kuwezesha kuupata huu uwanja wa nyasi bandia," alisema Majaliwa.

Timu ya Namungo, ilicheza mechi yake ya kwanza juzi usiku kwenye uwanja huo baada ya msimu mmoja kupita, ikishinda bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, lililowekwa nyavuni na Reliants Lusajo ambaye amefikisha mabao manne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.




Watoto wa Darasa la Awali wa Shule ya Msingi Minazini, Mwananyamala Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam, wakicheza mchezo wa ukuti wakati wa kipindi cha mapumziko shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Mfaransa wa Azam FC majaribuni Mbeya*

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Mfaransa Denis Lavagne, leo atatupa karata yake ya kwanza kuiongoza timu hiyo itakaposhuka dimbani dhidi ya Mbeya City kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Lavagne, ataanza kuiongoza timu hiyo ikiwa imeshacheza mechi tatu za Ligi Kuu msimu huu, ikishinda moja na kupata sare mbili matokeo yanayoifanya kushika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.

Kwa upande wa Mbeya City ipo nafasi ya saba ikiwa na alama nne baada ya kushinda mechi moja, sare moja na kupoteza mchezo mmoja kati ya mitatu iliyocheza hadi sasa kwenye ligi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria 'Zaka Zakazi', alisema kocha huyo amewataka wachezaji kujituma kupata pointi tatu huku akiendelea kukisoma kikosi chake hususan uwezo kila mchezaji.

"Kocha ndio kwanza amepewa kikosi, sasa hivi bado hajalijua vizuri soka la Tanzania, pia bado hajawajua wachezaji vizuri, hivyo atatumia mchezo dhidi ya Mbeya City kuwaangalia wachezaji na kupata kikosi chake.

"Kwa ujumla anahitaji pointi tatu katika mchezo wa kesho na amewataka wachezaji wajitume waweze kupata matokeo, na atakiongoza kikosi kwa jinsi alivyokikuta," alisema Zaka Zakazi.

Baada ya mchezo huo, Azam ambayo ina alama tano, itashuka tena katika uwanja huo Septemba 30, mwaka huu kuvaana na Tanzania Prisons.

Mbali na mechi hiyo, kesho kutakuwa na mchezo mwingine wa Ligi Kuu utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa Yanga iliyopo nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, kuikaribisha Mtibwa Sugar inayoshika nafasi ya pili nyuma ya vinara Simba, hata hivyo timu hizo tatu zinapishana tu kwa tofauti ya mabao kwani kila moja ina pointi saba.

# Michezo

Jumanne Septemba 13, 2022

Nipashe




Tuchel avunja ukimya kutimuliwa Chelsea UKURASA 21

FANYENI HIVI...



Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi, akitoa ushauri kwa washambuliaji wake, Fiston Mayele (kushoto) na Aziz KI hivi karibuni katika moja ya mechi za timu hiyo. **PICHA: MAKTABA**

## Mgunda sasa apiga mkwara mzito Simba

**Na Adam Fungamwango**

HUKU Kikosi cha Simba kikitarajia kuondoka jijini Dar es Salaam leo kwa ndege kuelekea Mbeya kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Tanzania Prisons, Kaimu Kocha Mkuu wa miamba hiyo, Juma Mgunda, amesema kazi ndiyo imeanza.

Akizungumza juzi usiku baada ya kuwasili kutoka nchini Malawi kucheza mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika Jumamosi, ambayo walishinda mabao 2-0 dhidi ya Nyasa Big Bullets, Mgunda alisema matokeo hayo wameyasahau kwa muda na sasa akili yao ni kwenye mechi ya raundi ya nne ya Ligi Kuu dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya kesho.

"Mechi ile imekwisha, sasa tunafikiria mechi inayokuja, tutakwenda kucheza mechi ya ligi Jumatano, nitakutana na uongozi na benchi la ufundi kuona nini kinafanyika, halafu kesho (jana), tutafanya mazoezi kwa sababu hatuna muda, tunafikiria ya Mbeya kwanza, ni muhimu sana kwetu kushinda, tukiimaliza mechi hiyo ndiyo tutaanza kufikiria mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema.

Mgunda alisema ushindi uliopatikana nchini Malawi umekuwa chachu kubwa, huku akiwapongeza wachezaji, viongozi na mashabiki wa klabu hiyo kwa kuwapa sapoti kufanikisha kufanya vema ugenini.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema ushindi walioupata ugenini umeiheshimisha nchi.

"Ukienda kwenye nchi za watu na kwenda kumfunga bingwa mbele ya mashabiki wao ni fahari kubwa, vijana wameiheshimisha klabu na nchi kwa ujumla," alisema.

# Yanga yamwagiwa bilioni 10/-

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

## Mambo yazidi kunoga ikiivaa Mtibwa leo, Nabi sasa aanza kulia na ratiba...

WAKATI uongozi wa Klabu ya Yanga ukitangaza kuongeza mkataba na mdhamini wao, Kampuni ya GSM, utakaokuwa na thamani ya Sh. bilioni 10.9 kwa kipindi cha miaka mitano, Kocha Mkuu wa Mabingwa Watetezi hao wa Ligi Kuu Bara, Nasreddine Nabi, amelia na ratiba kubana kuelekea mchezo wao wa leo dhidi ya Mtibwa Sugar.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema wameingia makubaliano ya kusaini mikataba miwili ukiwamo wa udhamini wa jezi na vifaa vingine vya michezo wenye thamani ya Sh. bilioni 9.1 kwa kipindi cha miaka mitano ambapo kila mwaka watapokea Sh. bilioni 1.5 na ongezeko la asilimia 10 kwa kila mwaka.**

Alisema mkataba wa pili wa udhamini wa klabu hiyo ni wenye thamani ya Sh. bilioni 1.8 na kila mwaka watakuwa wakipokea Sh. milioni 300.

"Baada ya makubaliano ya pande zote mbili tumeingia mkataba wa miaka mitano na Kampuni ya GSM wenye thamani ya Sh. bilioni 10.9 baada ya ule wa awali kufikia tamati.

"Mkataba wa awali ulikuwa ni Sh. milioni 150, ambao ulikuwa wa haki za matangazo na sasa ni Sh. milioni 300 kwa mwaka mmoja, lakini pia kuna vipengele vya asilimia 10, mkataba wa pili unahusu vifaa ikiwamo jezi, hivyo jumla ya udhamini huo ni Sh. bilioni 10.9," alisema Hersi.

Mkurugenzi wa Masoko wa GSM Group, Allan Chonjo, alisema wanafuraha kubwa kuendelea kuidhamini Yanga kwa mara nyingi kutokana na ukubwa wa klabu hiyo.

"Tunapenda kushukuru Wanayanga kwa kuleta maendeleo katika klabu, lakini Watanzania wote katika kuendeleza michezo kwa Tanzania na kufanikiwa kwa asilimia kubwa kuleta vifaa bora katika masuala mbalimbali ikiwamo jezi," alisema Allan.

Hata hivyo, wakati uongozi ukitangaza neema hiyo, Kocha Mkuu, Nabi amelia na ratiba ya Ligi Kuu kubana na kuathiri timu zote zinazoshiriki mtifuano huo sambamba na mashindano ya kimataifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Nabi alisema mechi zinapokuwa karibu karibu zinafanya wachezaji wasiwe na kiwango kizuri mchezoni.

"Michezo kupangwa karibu karibu haiziathiri timu pekee zinazoshiriki mashindano ya kimataifa, bali huathiri timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu kwani hazipati muda mrefu wa kupumzika, wachezaji wanatakiwa wapate muda wa kutosha kupumzika," alisema Nabi.

Kuhusu maandalizi kuelekea mchezo wa leo dhidi ya Mtibwa Sugar, aliwataka wachezaji wake wajitume kwani wapinzani wao hao wana wachezaji wazuri.

"Timu yangu mpaka sasa bado haijakuwa na muunganiko mzuri, hii imetokana na kufanya mazoezi na wachezaji nusu huku wengine wakiwa kwenye majukumu ya timu ya Taifa (Taifa Stars), naamini siku zinavyozidi kwenda itakuwa na muunganiko mzuri," alisema.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadhi Juma, alisema: "Hatuhofii kukutana na Yanga, japo msimu uliopita walikuwa mabingwa hatuna shaka kukutana nao."

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >